Hili, pia, linatambulika mu sura ile ya kwanza kabisa ya *Kuelekea mu Maono ya Pamoya*, na kote kote kwa maandishi. Kusema kuwa "Kanisa ni uhalisi wa kiungu na kibinadamu" (23, k. 14) ni kusema kuwa kando ya ufahamu wetu juu ya kanisa kuwa zawadi kwa Mungu wa Maumbile,"kiumbe cha neno la Mungu na roho mtakatifu."[22] Lazima tuweze kuweka ufahamu yenye ili na uwazi sawa juu ya kile chenye uhalisia wa binadamu una ashiria. Lazima, mu theolojia yetu sisi wenyewe, tuweze kujihusisha na kuelewa matumizi ya binadamu mu kanisa.

Kama mila nyingine ya dini na jamii, makanisa ya Bakristo kuhudumu mu mahitaji mseto ya binadamu na makusudio, ku njia zenye zina tofautiana pakubwa ku fasi moja na muda mwingine. Zinahudumu kwa pamoya mu mahitaji ya binadamu juu ya mpangilio, utangamano, kujizuwia, utiliaji mkazo wa imani, urafiki, mwongozo, na mengine mengi. Banaathiriwa kwa kila sehemu na njia halisi za binadamu kutangamana wenyewe kwa wenyewe mu matoshelezo ya mahitaji yao. Zinaweza pia kutumika mu huduma za faida mengine kwenye sehemu ya vishikanishi na "batu ba inje" vile vile, kwa mfano, kwa kufanya kuhudumu kwa hatima fulani za kisiasa na kiuchumi. Hakuna mtu mwenye alizoweana na historia hii ya makanisa ya Bakristo tangiya karine za mapema sana kuenda mbele anaweza kushindwa kutambua mwingiliano huu mgumu wa mahitaji ya binadamu, matamanio, maono, na woga mu historia hiyo. Wakati mwingine ni rahisi sana kutambua elementi hizo mu maisha ya kanisa mu bamingi fasi nyingine na muda kuliko nyingine binafsi.

Bamingi matumizi haya ya pamoya ya binadamu inakuwa wazi kabis katika uendelevu wa misheni binafsi ya kanisa kama ishara na huduma ya*koinonia*. Mu prametre hizi, tunaweza sema kuwa shabaha ya Mungu na shabaha ya batu, kukutana na mahitaji sahihi ya batu na mu huduma ya kuishi-muzuri kwa viumbe vya Mungu. Katika hali kama hizo, tunaweza kusema kuwa

---

[22] *Maumbile na misheni ya kanisa*, Karatasi ya 198 ya Maneno ya Mwenendo na Imani ya Kanisa (Geneva: Baraza la Makanisa Duniyani, 2005), 9, k. 13. Karatasi hii ilikuwa, kama vile kichwa chake kidogo kyenye kinaonyesha, utangulizi wa maandishi ya 2013: "jukwaa lenye lilikuwa mu njia ya kauli ya pamoya."

kusudio la Mungu na makusudio ya binadamu ni bitu byote byenye bimepangiliwa pamoya, mu mukutano halisi wa mahitaji ya binadamu na mu huduma ya hali—njema ya uumbaji wa Mungu, mifano mingine, matumizi ya binadamu inaweza kuwa katika mgogoro wa moja kwa moja na kusudio la kiungu—kwa mfano, wakati kanisa linahudumu, haijalishi kama ni kwa werevu au ni kwa makusudi, kama chombo cha idiolojia ya kitaifa, kirangi, kikabila, au ubabe wa jinsia. *Kuelekea Maono ya Pamoya* anataja mseto mmoya wa matumizi mabaya kama haya: "Wakati mwingine, torati ya kitamaduni na kidini ya bale batu benye injili imetangaziwa habakupewa heshima yenye balista hili, kama bale benye banajihusisha mu mambo ya uinjilisti balikuwa habaungi mkono ukoloni mambo leo, yenye yalitokana na batu benye bali ondolewa na basiweze kujitetea bao benyewe zidi ya mataifa yenye nguvu yenye ina bashambulia " (6, k. 7). Kwenye myaka yenye ilipita, Kanisa Methdosite Umoja limeweza kupewa ufahamisho mpya juu ya historia yake yenyewe yenye haikuwa huru zidi ya uhusishwaji na matukio ya aina fulani, hata kama tungependa kukumbuka mpakathi zenye furaha sana.[23] Ili kutoa sehemu hizo za simulizi juu ya historia yetu yenye ilipita (na ya sasa) yenye haionyeshi vizuri sana juu yetu ni kujidanganya pamoya na bale batu beninge, na hali hii inatuacha sisi tukiwa katika hali-mbaya juu ya utambuzi wa makinifu wenye unahitajika na mwito wetu. Mu utambuzi huu, maono ya zawadi ya *koinonia* yenye ni mapenzi ya Mungu juu ya kanisa mu nyakati zote na fasi zote ni sehemu muhimu ya marejeleo.

## Jamii ya Wokovu na jamii kama Ishara

*Mapendo ya kuokowa ya Mungu yamenuiya batu bote*. Biblia haiweki wazi mfumo mmoya wa kawaida ao uelewa wa kanisa. Hakuna mwongozo kamili mu Agano Jipya wenye unafaa kufuatwa. Hata hivyo, maandiko inatupa mali nyingi juu ya kufikiria kwetu juu ya njia zenye Mungu anafanyia kazi ili kuanzisha au kurejesha mawasiliano ya karibu na miongoni mwa wanadamu. Bamingi picha hizi za maandiko na hali zimekuwa na wajibu wenye ushawishi mu historia ya Bakristu mu fikira na matendo, ijapokuwa uzito yenye inatolewa ku picha fulani zenye zinaongoza umetegema kutoka wakati mmoya na fasi moya na nyingine. Bengine bamepokea umakinifu kidogo kwa kiasi fulani. Batatu ku bale benye ushawishi mkubwa sana—"batu ba Mungu," "mwili wa Kristu," "hekalu ya Roho Mtakatifu"— byote bimeweza kutajwa mara kwa mara na kuchunguzwa mu mazungumzo ya kisasa ya umoya wa madini, kwa kiasi fulani ju ya njia zenye tofauti zabo zinachochea kufikiria kwetu. Kwa pamoya, binasaidia

[23] Maombi ya 3323, "Uhusiano wa uponyaji pamoya na batu benyeji," na namba ya vitendo vya kumbukumbu na kukiri yenye yametekelezwa mu muunganisho nayo, ni ishara ya tumaini juu ya ufahamisho huu mupya. Angalia *Kitabu cha Mipango 2012 cha*, kk. 419-420.

kutilia mkazo hoja kuwa*koinonia* ni zawadi ya Mungu muumbaji, na pia kuwa utambuzi wetu ku na mwitikio wa zawadi hiyo unaweza kuchukua mifumo tofauti. Yenye ina mwaliko yenye ilichaguliwa ili kuchunguza utajiri na mseto wa picha, istiari, na mawazo yenye baandishi ba biblia bailtumia kuonyesha bahusika ba jamii mupya yenye Mungu anaumba.

Neno lingine la kipekee, lenye kuandamana bamoya na picha kama bile bale batatu vile alitaja hivi punde, linaweza kutoa mtazamo wa matumaini ku mseto wa maana wa “kanisa” na mifumo mingi yenye inaweza kuchukuliwa nayo njo yenye inatumika mara kwa mara mu Agano Jipya ili kupangilia jamii ya Bakristo: *ekklesia*. Mara nyingi inachukuliwa kuwa “kanisa” mu tafsiri za Kiingereza ku Agano Jipya,[24] ni “jamii” (*Gemeinde*) mu Agano Jipya la Kijerumani la Luther’s, huku lugha zitokanazo na Kilatino inabakiza kitu mu tafsiri na muunganisho wa Kilatino, *eklesia*, kama vile mu Kifaransa *éklise*, Kihispaniola *iklesia*, ao Kiitaliano *chiesa*. Mu nyakati za Agano Jipya na ku bamingi karne mbele ya, *ekklesia* kulikuwa na neno la Kigiriki la bamoya juu ya gwaride au kusanyiko, kama vile mukutano wa banainchi benye bana chagula mu taifa la jiji la Kigiriki. Pia ni neno kwa kawaida lenye linatumika mu tafsiri ya Kigiriki ya maandiko ya Kihibrania, ile Septuagint, ili kutafsiri neno la Kihibrania *qahal*, vile vile neno la kijeneriki kumaanisha mikutano au kusanyiko—mukutano wa kidini, kwa mfano, ao mseto wa kijeshi yenye ili tayari kwa vita. Moya wapo ya matumizi ya kudumu sana ya *qahal/ekklesia*, mu Bakristu ba mapema bamoya na kumbukumbu ya Bayahudi, ilikuwa katika muunganisho wa gwaride la batu pale Sinai wakati Toraa inatolewa (“siku ya gwaride,” Deuteronomy 18:16) Kumbukumbu ya torati na kwa matarajio ya furaha ya hatimaye na kusanyiko la ukombozi la batu ba Mungu, kama ilivyo fafanuliwa mu mufano wa Isaya 25:6-9. *Ekklesia*, kisha, mu akili ya mwandishi kama vile Paulo, alikuwa na mseto wa manufaa. Angerejelea jamii fulani ya batu ba nyumbani mu Bakristo ao kwa pamoya ju ya jumla ya jamii kama hizo za nyumbani, ao ku batu bote ba Mungu mu nyakati zote, na fasi zote (“Kanisa la duniyani muzima,” kama vile vile inaitwa wakati mwingine).

[24] “Kanisa” haswa linatokana na neno jingine la Kigiriki, *kyriake*, “kumilikiwa na Mungu,” lenye halikuwahi kutumika mu Agano Jipya ili kurejelea jamii ya Bakristo. Matumizi haya yalijitokeza ku mwisho, na hatimaye yakajipata mu Kiingereza. Bamingi tafsiri za Kiingereza za mapema, haswa zile za William Tyndale ziliweza kuishughulikia *ekklesia* kama “baumini” pahari pa “kanisa”—chaguo lenye maagizo ya kifalme ku batafsiri ba toleo la King James baliweza kutolitilia maanani katu.

Maneno yote “kutaniko” na “kusanyiko,” pamoya na “mukutano,” “baamini,” na bamingi maneno mengine yenye yamefanyizia kazi mu nyakati tofauti ili kushughulikia *ekklesia*, ina bamingi unyumbukaji wenye kivutio: inaweza kurejelea kitendo au mchakato (kuja pamoya, kufanya kuja pamoya), ao ku kundi lenye linaundwa, ao ku bamemba ba kundi hilo haijalishi kama bataweza kusanywa pamoya kwa muda huu au la. Bado, Luther—akitarajia namba ya bakalimani ba siku ya-leo—pengine aligonga njo: kisawe chenye ubora sana wa kisasa cha *ekklesia* mu mawazo wa mu Kristu unaweza pia kuwa “jamii.” Hali hii inashawishi haswa kama tutatilia maanani kufungwa kwa miunganisho kati ya mada ya kusanyiko (*ekklesia*) na mada ya mawasiliano ya karibu (*koinonia*).[25] Miongoni mwa binadamu, mawasiliano ya karibu huchukua mfumo wa jamii.

*Eklesia* yenye ina mtazamo wa ziada juu ya nyuzi fulani za mila ya Kiporo zenye zimeunda Methodiste Umoja. Miongoni mwa viwango vya falsafa ya Kanisa Methodiste Umoja ni misemo ya dini yenye ili letwa mu ya muungano na Kanisa Methodiste na kukiri kwa imani kuliyo letwa mu yake na Kanisa la Bandugu la Umoja wa Kiinjilisti. Kila moya lyenye ina msemo wa kanisa, kando kando na kanda mengine yenye inafaa juu ya mada husika. Misemo miwili mikuu ni hii:

Kwanza, kutoka kwenye Misemo ya Dini, Msemo wa XIII—Wa Kanisa:

> Kanisa lenye linaonekana la Kristu ni baamini benye banaume baaminifu penye neno safi la Mungu linahubiriwa, na Sakramenti kuweza kutolewa vilivyo kulingana na mpangyenye ili wa Kristu, mu mambo hayo yote yenye ina hitajika ya lazima inafanywa vivyo hivyo.

Na kutoka kukiri kwa Imani, Msemo wa V—Kanisa:

---

[25] Kutafakari kwenye manufaa ju ya matumizi ya *ekklesia* kunaweza kupatikana mu Paula Gooder, “Kwa Utafutizi wa Kanisa ‘la Mapema’: Agano Jipya na maendelo ya jamii za Bakristo za mu Kristu,” *Mbia wa Routledge ku kanisa la mu Kristo*, ilihaririwa na Gerard Mannion na Lewis S. Mudge (New York and London: Routledge, 2008), kk. 9-27, mu ya Gordon W. Lathrop, *Batu Batakatifu: Masomo ya Kanisa ya Kiluturujia* (Minneapolis: Fortress Press, 1999), kk. 21-48.

> Tunaamini Kanisa la Kristu ni jamii ya baumini bote ba kweli chini ya Ubwana wa Kristu. Tunaamini ni moya, takatifu, lenye utume na la kikatoliki. Njo ushirika wenye neno la Mungu linahubiriwa na banaume benye balitwa kwa Kiungu na sakramenti zinatolewa vilivyo kulingana na uteuzi binafsi wa Kristu. Kwa uongozi wa adabu ya Roho Mtakatifu Kanisa linakuwepo juu ya kuendeleza kuabudu, urekebishaji madili ya baumini na ukombozi wa duniya muzima.

Ufazili wa kwanza, kutoka mu misemo ya Methodiste, ni kwanza kabisa utoaji upya wa msemo linganifu wa (XIX) mu Misemo Makumi tatu na tisa ya Kanisa la Uingereza (1563), kutokana na musemo wa VII wa Imani ya Kilutheri kwa Augsburg (1530). Unatambulisha kanisa (*eklezia*, mu tole la Kilatino na Kianglikana na maandishi ya Kilutheri) "kama baumini ba banaume baaminifu" ("na banamke," tunaweza kuongezea kuwa kweli hali halisi leo, ao tunaweza kushughulikia *coetus fidelium* kwa uwazi sana kama "baamini ba baaminifu"), benye bali kusanyika na juu ya Neno na Sakramenti. Ingawaje bamingi falsafa za kimapokeo za Protestanti za kanisa zinatoa uhakika wake wa kimsingi hapa na hitimisho kuwa kunazo "alama mbili muhimu" za kanisa—utangazaji halisi wa neno, na usimamizi bora wa Sakramenti—batu bengine banatambulisha alama tatu kama hizi: kuongezeya ku neno na Sakramenti, ipo alama ya waaminifu wenyewe, ao uanafunzi, ao adabu, ao maisha ya pamoya yenye ili ongozwa na ahadi za Mungu. Ni mradi huu wa ku mwisho wenye, kutoka ku upande wa Protestanti, yenye ina ingia kwenye uelewa wetu wa umoya wa madini wa muundo au kuwepo kwa watatu mu maisha na misheni ya kanisa.

Utafsiri wa pili, ukiangazia torati ya Bandugu wa Pamoja wa Kiinjilisti, yenye ina elementi za kimsingi za ile ya kwanza lakini yenye yenye ilingezwa laza mu njia tofauti. (Kuhusiana na "banaume baaminifu" ba Utafsiri wa kwanza, leo tungependa kusema kuwa neno linahubiriwa na "na banamke na banaume benye baliitwa kwa njia ya

kiungu" ao "batu benye baliitwa kwa njia ya kiungu." Kauli ya ku mwisho inatumika kama kifungo wa msemo huu na inaingizwa mu ya Utafsiri wa kanisa la mu mu *Kitabu cha Mwenendo 2012*, ¶201). Inafanya wazi wazi sana kipengele cha jibu la uaminifu—alama "ya tatu"—kukiwa na maneno kama "ushirika wa ukombozi" na marejeleo ya misheni ya kanisa, na pia inahusisha vivumishi kutoka kwenye taarifa ya imani ya Nicene yenye inatambulisha kanisa kama "moja, takatifu, yenye mitume ya apostoliki na la katoliki."

Sifa ya kutaja juu ya msemo wa kwanza yenye ilinukuliwa—na, kwa ufafanuzi, wa pili, yenye inajengewa juu yake—ni kuwa unatoa Utafsiri wa*kanisa* lenye linaonekana. Utofautishi kati ya "kanisa linaoonekana" na "kanisa lenye halionekana" ulikuwa maarufu wakati wa Marekebisho ya Protestanti, huku mizizi ikienda nyuma kule sana. Kama vile inaeleweka ku mazoea, kanisa lenye linaonekana lilikuwa jamii halisi, baumini ba mu ba Bakristu benye banakiri, au kundi kubwa sana lenye linaweka pamoya baumini bengi ba mu, benye banasikia na kuthibitisha Neno kwa lenye kuhubiriwa kwa usahihi, na kuchukua sakramenti na kuunga mkono huduma ya kanisa. Kanisa lenye hali onekana lilieleweka kuwa jumla ya batu benye bameokolewa kwa hakika, ao benye bako mu njia ya wokovu. Kampuni hii "haiyonekani" kwa maana ya kuwa hakuna yeyote ila Mungu anayejua kwa uhakika ni nani aliyehusishwa mu yake. Ilichukuliwa kwa njia maarufu (na mara nyingi ikatiliwa mkazo na banathelojia na bahubiri) kuwa kwa kutorejelea mambo machache bamemba ba kanisa lenye halionekana lenye lyenye ilikolewa kwa kweli, balikuwa tu Bakristu benye banakiri, bamemba ba kanisa lenye linaonekana; lakini kuwa kanisa lenye linaonekana pia linazo (kutumia maneno ya John Calvin) "mseto mkubwa sana wa batu banafiki, benye haba na chochote juu ya Kristu lakini jina na mwonekano wa inje."[26]

Mitazamo ya Bakristo bengi na jamii nyingi za Bakristu juu ya swala hili imebadilika mu miaka ya hivi majuzi. *Kuelekea maono ya pamoya* (25, k. 15) inawakilisha uvutaji pamoya mpana sana, ingawaje yenye inaonekana, hapa miongoni mwa makanisa yenye inahusika, ku kikundi ya umoya wa madini:

[26] John Calvin, *Anazungumzia juu ya dini ya Kikristu*, kanda yalitafsiriwa na Henry Beveridge (London: James Clarke, 1962), kanda ya 2, k. 288 (IV, 1, 7).

> Juu Mungu ana mapenzi kwa batu bote kuweza kuokolewa na kufikiya kuyuwa ukweli (rejelea. 1Tim 2:4), Bakristo banatambua kuwa Mungu anabafikia bale benye habakuwa bamemba ba wazi wazi mu kanisa, mu njia zenye si za kuonekana mara moja na macho ya binadamu. Huku bakiheshimu vipengelee vya ukweli na wema vile ina patikana mu madini mengine na mu mwa bale benye habakuwa na dini, misheni ya kanisa inabakia ile ya kubaalika, kupitiya ushuhuda na ushahidi banaume na banamke bote kuja kuyuwa mapendo ya Yesu Kristu.

Kile chenye taarifa kama hiyo inaruhusu ni uwezekano kuwa batu benye habakuwa "bamemba ba wazi wazi" banaweza pia kuwa, kiasi fulani bamemba ba kanisa, bashiriki mu ile *eklesia* moya ya Mungu, batumizi mu mawasiliano ya karibu yenye Mungu anatoa. Kumbuka kuwa kauli hiyo haipendekezi kuwa batu bote ni, kwa hakika kwa kuitikila mapendo ya Mungu mu njia kama hiyo, wala haya ashirii kuwa bale benye banafanya hivyo banaitikia na bao hivyo basi ni "Bakristu ba kweli" bila ya kujua. Inaweza, hata hivyo, kuashiria kuwa *koinonia* ya Mungu inaweza kuwepo mu mifumo mingine na fasi nyingine. Kama Mungu anafikila kwa bale benye bali sana ya jamii zetu za Bakristu mu njia zenye zinafichwa kwetu sisi, na kama banaitikila mapendo ya Mungu kwa njia muzuri, basi pengine tunahitaji hali kubwa sana ya "kanisa" kuliko ile tuliyozoea kutumia. (Kama vile Irenaeus vile alisema kitambo, "pale roho wa Mungu alipo, kanisa lipo na neema yote.") Kanisa, kwa maana ya ile moya ya *eklesia* ya Mungu, jamii ya wokovu, yenye haina mazingira mamoya na makanisa tunayoyajua. Makanisa hayo tunayoyua inashiriki mu hiyo *eklesia*kubwa sana (hata hivyo kwa njia yenye kasoro), lakini kazi yao maalum ni kuweza kuweka ishara wazi wazi, na kuhudumia utoaji—nafsi wa kipekee wa Mungu ku mwanadamu kuweza, kama bamingi mila itakavyotaka kusema kwa njia ya kimaumbile, sakramenti—kupitiya kwa kuabudu kwao kwa Mungu, matunzo yao na maumbile ya bale benye banakuya ku imani kupitia kwa ushuhuda wao, na huduma yabo ku mariziano ya Mungu na kusudio kombozi.

Makanisa inatekeleza kazi hii benye balipatiliwa tuseme kwa njia muzuri. Kwenye maneno halisi ya kukiri kwa Westminster, kanisa “limeweza wakati mwingine kuonekana sana, wakati mwingine kutoonekana sana” mu jamii zile zenye zinajiita makanisa.[27]

John Wesley alilalamikia hoja kuwa Bakristo bengi benyue kiri ba siku hii benye balinekana kwa njia bora sana kuwa na “mfumo wa utakatifu, lakini si balikosa nguvu za kuandamana na utakatifu huo” (rejelea. 2 Tim 3:5), si juu ya Mungu kuweza kuwa alikariri kutohusishwa kwabo mu wokovu, lakini juu ya abo kukatala kutumia neema benye balipewa na Mungu mwenye “kutaka batu bote kuokolewa” (1 Tim 2:4). Wakati huo huo, Wesley hataki kuamini kuwa umati wa batu benye balikuwa *ule yenye haikiri kuwa* Bakristo—kwa mfano, namba kubwa ya batu maskini mu Uingereza balikuwa bametengwa na kanisa na balihisi kutohusishwa na kanisa, ao batu bamilio ni mu duniya muzima benye balikuwa habajasikia juu ya injili, baliimwa kabisa neema ya Mungu juu ya hayo, kwa sababu zenye zinakuwa sana ya kujizuwia. Kinyume cha mambo, alisha-wishika kuwa Kristu alibafia batu bote, kuwa hatia ya zambi ya mu yenye batu banaweza kuwa balijipata nayo kupitiya kwa kuanguka kwa bazazi betu ba kwanza ilikuwa imefutiliwa mbali kwa batu bote, na kuwa neema ilipatikana juu ya wote. [28] Funzo lenye tunaweza kujifunza kutoka ku Wesley ni kuwa tunahitaji kwa mkono

---

[27] Kukiri kwa Imani kwa Westminster, 25.4.

[28] “Sina mamlaka kutoka ku neema ya Mungu ‘kuhukumu bale benye habakuwa nacho’ [msemo wa Bakristo]. Wala sielewi kuwa mutu yeyote ailye hai ana haki ya kubahukumu batu bote kafiri na ulimwengu wa batu ba Mahometan juu ya moto wa Jihenamu. Ni bora sana kubaacha batu abo kwake, yeye alibaumba, na aliye ‘baba wa roho za mwili wote’; aliye Mungu wa makafiri pamoya na Bakristo, na asiyechukia chochote chenye alikiumba. . . . [K]ama moyo wa mwanadamu utajazwa (na neema ya Mungu, na nguvu za roho wake) kwa upendo wenye unyenyekevu, mtulivu, wenye subira juu ya Mungu na binadamu, Mungu hatamtupa mu moto wa milele uliyo tayarishiwa Shetani na malaika wake juu ya mawazo yake kutokuwa wazi au juu ya zana zake zenye zina na mkanganyo.” “Juu ya kuishi bila ya Mungu,” *Mahubiri ya IV*, imehaririwa na Albert C. Outler, *Kazi za John Wesley*, kanda ya 2 (Nashville: Abingdon Press, 1987), kk 174-175. Mu mchango wake juu ya Vitendo 10:34-35—“Kisha Petro akaanza kubaongelesha: ‘Naelewa kwa kweli kuwa Mungu hana upendeleo. Lakini mu kila taifa yeyote yule anamcha yeye anafanya wa maana na wa kukubalika na yeye’”—mu *Nakala zake juu ya Agano Jipya*, Wesley aliandika: “Lakini mu kila taifa yule ana mcha Mungu na kujitakasa - Yule yule ana, kwanza, kumstahi Mungu, na kumwona kuwa mkubwa, mwenye hekima, mzuri, mwenye sababu, hatima, mtawala wa mambo yote; na pili kutokana na kumchukulia kwa hali hii mbaya, hajiepushi tu na maovu yote yenye inajulikana, lakini analenga kulingana na mwangaza bora sana wenye anao, kufanya mambo yote vyema; anakubalika na Yeye - kupitia kwa Kristu,

mmoya, kuendeleza uwezo wa kihalisia na wa kuchunguza nafsi zetu tunapokuya ku ubora wa maisha yetu binafsi na kushuhudia kama Bakristo na jamii za Bakristo, kuwa macho juu ya hatari za udanganyifu wa nafsi na kuwa na habari juu ya mahitaji yetu ya kudumu juu ya toba na maisha mapya; na, kwa mkono mwingine kuwa wazi mu uwepo wa Mungu mu majirani zetu, bakiwemo benye habakuwa-Bakristo, na kuwa wazi mu mapendo ya Mungu yenye inaweza kuya kwetu kupitia kwabo. Mukao kama huo ni unaweza, kwa hakika kuonyeshwa mu mafunzo ya Methodiste Umoja kuhusiana na mahusiano yetu kwa bale bengine ba mila ya kidini. [29]

Kuongelea juu ya kanisa la Bakristo kwa ujumla—mumaandishi ya umoya wa madini, hii ni kawaida mu “Kanisa” likiwa na herufi kubwa “K”—*Kuelekea Maono ya Pamoya* inatoa ufafanuzi wenye manufaa na msaada (mu 22, kk. 13-14) juu ya ukujaji pamoja wa umoya wa madini juu ya “alama” zile inne za Nicene zenye zilitajwa mu kukiri kwetu kwa imani zenye zinaweza kueleleweka. “Kanisa ni moya ju Mungu ni mmoya (rejelea. Yohana 17:11, 1 Tim. 2:5). . . . Kanisa ni takatifu juu Mungu ni mtakatifu (rejelea. Is. 6:3; Lev. 11:44-45).” Kanisa ni katoliki juu Mungu taka kuwa la batu bote duniya muzima. Kanisa ni la mitume juu ya asili yake mu ushuhuda yenye ilitumwa (mutume ni “yule mwenye ali tumwa”) na Mungu wa Utatu na mwito wake “kuwa mwaminifu siku zote kwa asili zile za kitume.” Mu kila mufano, maandishi inatilia maanani kuwa utendakaji wetu halisi unapungukiwa: tena, uhalisia wa kiungu wa kanisa “wakati mwingine huonekana sana, wakati mwingine hauonekani sana” mu halisi wake wa kibinadamu.

“Mseto wa kihalali mu maisha ya mawasiliano ya karibu ni zawadi kutoka ku Bbana” (28, k. 16). Hakuna marejeleo ku “kanisa” kwa umoya inafaa kuchukuliwa ili kuashiria kuwa tofauti hazina mahali mu jamii ya Kikristo. Hoja kuwa Mungu wa Utatu ndiye chanzo cha mawasiliano yetu ya karibu, inafaa kuwa tosha kutukumbusha sisi kuwa ni umoya mkuu, wa kimahusiano, wala si upamoya wa upande mmoja wenye kutafutwa. Zawadi za Roho zinatofuatiana mu tabia (1 Wak. 12:4-7) na byote

---

hata kama hamjui. Utiliaji maanani huu ni wa moya kwa moya na hauruhusu kutumuisha kokote. Yeye yumo Mukibali cha Mungu, haijalishi kama anafurahia neno lake kwa maandishi pamoya na sheria husika au apana. Hata hivyo kuongeza kwa haya ni baraka yenye sitamkika kwa bale wenye awali Mu hali fulani baliweza kubalika. Vinginevyo Mungu asingewahi kumtuma malaika kutoka mbinguni ili kumwelekeza Cornelio mpaka Mt. Petro.”

[29] Cf. “Tumeitwa ili kuwa majirani na mashahidi: Miongozo ya mahusiano ya aina ya dini,” *Kitabu cha Mipango cha 2012*, kk. 269-279.

binaonyeshwa mu njia tofauti kwa mema ya pamoya. Pia, binadamu na tamaduni zabo banatofautiana kutoka mmoya mpaka mwingine mu njia tofauti, na tofauti hizi zinapatia nguvu *koinonia* yetu. Makanisa halisi fulani—baamini ba ndani, mila ya kihistoria ya Bakristo na nyuzi zake mbalimbali na bikundi ya mpangilio—byote bimeweza kuonyesha njia zake za kibinafsi za kuwa kanisa. Ziko huru kutofautiana, na kwa mingi kiwango lazima zitofautiane, ili kuweza kuhusiana mu hali mbali mbali zenye zinajipata ndani na ili kutambua zawadi zabo kabisa. “Mseto wa kihalali unakosa kumakinikwa kila wakati Bakristo benye banachukulia maonyesho yabo binafsi ya kitamaduni ya injili kama yale yenye ni halali, na yenye inafaa kulazimishwa juu ya Bakristo ba tamaduni nyingine” (28, k. 16).

Namna gani mseto halisi unaweza kutofautishwa na mseto usio halali ni swala lenye lingali linatafuta jibu wazi mu muktaza wa umoya wa madini, kama *Kuelekea Maono ya Pamoya* venye inahakikisha (30, kk. 16-17). Kanuni yenye kizahania inaweza kukubaliwa, kama vile ule mseto usio wa halali ulivyo ule yenye inazalilisha umoya wa kanisa; lakini njia ya aina hii inaweza kutumiwa vibaya kwa urahisi. Mchango juu ya swala hili, maandishi inatafakari ni nini chenye kinaweza kuhitajika:

> Hata kama makanisa yote ina taratibu zake binafsi za kutofautisha mseto wa halali na zidi ya ule usio wa halali ni wazi kuwa mambo mawili inakosekana: (a) mpangilio wa pamoya ao mbinu za utambuzi (b) miundo kama hiyo yenye ilitambulika kwa pamoya kama venye inahitajika kwa matumizi yake ya kikamilifu. Makanisa yote inatafuta kufuata mapenzi ya Bwana, ilhali inaendelea kutokubaliana na hali mingi za imani na mwenendo na, vile vile, juu ya kama kutokubaliana kama huku inapotosha-kanisa ao, pahari pake, ni sehemu ya mseto wa halali. Tunai alika makanisa kuweza kutilia maanani: ni hatua gani mbili zinaweza kuchukuliwa kwa kutoa utambuzi wa pamoya yenye inawezekana?

Kama vile maandishi inatambua chini kwa chini nyuma ku (63, k. 35), ni kauli yake hapa yenye inasema “makanisa yote ina taratibu zake binafsi za kutofautisha mseto wa halali na ule wenye si halali” na

huenda si sahihi kwa ujumla. Kunaweza pia kuonekana kuwa na hukumu tofauti *ndani ya* idadi kazaa ya makanisa kwa sasa juu ya hoja hii hii—yaani kuhusiana na utofauti fulani ni kwa falsafa au kwa mwenendo unahusisha mseto wa halali au la—na hakuna mbinu zozote za kufanya kazi za kutatua ulizo hili. Mu hali kama hiyo, mambo ile inaweza kuhitajika kuwa maandishi inapata kuwa na ukosefu mu mawazo ya umoya wa madini: “(a) mpangilio wa pamoya, ao mbinu za utambuzi, na (b) miundo kama hiyo tambulika kwa pamoya ipo kama venye inahitajika ili kutumia hivi kwa njia bora.” Kanisa lenye linajipata mu hali hizi huenda likahitaji kujiuliza swali lile lile lenye maandishi haya inaulizia ku makanisa kwa pamoya: Ni hatua gani nzuri zenye zinaweza kuchukuliwa ili kuwezesha utambuzi wa pamoya? Mu kutatua ulizo hili, kila kanisa linaweza kusaidiwa kwa kuingila mu mazungumzo ya umoya wa madini juu ya mada haya, kujizoesha na mitazamo yenye makanisa mengine yamefanya ili kutambua mipaka ya mseto husika, kujifunza kutoka kwenye uzoefu wabo, na kuchunguza-upya mtazamo wake binafsi kwa mujibu wa hayo yote. Tutarejelea swali hili hapo nyuma.

## Imani, Tumaini, na Mapendo

*Mapendo yenye inaokowa ya Mungu ni ya kubadilisha*. Tabia namwelekeo wa mabadiliko hayo byote bimewekwa mu sehemu ile yenye ili zoeleka ya Pauline, “imani, tumaini, na mapendo” (1 Wak. 13:13). John Wesley na mila yetu ya Kimethodiste bila shaka angetilia mkazo uhakikisho wa Paulo kuwa “kubwa sana kati ya hizi ni upendo.” Lakini si Wesley wala sisi tungependa kupuuza vipengele vile viwili vingine vya utatu. Byote bitatu ni muhimu, na bina uhusiano wa ndani kwa ndani. Kunacho kile kipengele cha utatu—ao, tukisema kwa njia muzuri—yenye utatu—tabia yenye inahusu maisha yenye Mungu anapatia jamii, na juu ya sababu hiyo kuna tabia ya utatu ao Yenye Utatu juu ya namuna kanisa inajionyesha mapendo ya Mungu mu duniya muzima.

Haishangazi, hivyo basi, kuwa kote kote mu sura za *Kuelekea Maono ya Pamoya* kuna mafafanuzi ya utatu yenye inajitokeza juu ya ile kanisa limeitwa kuwa na kufanya. Kwa mfano, Mu ufafanuzi wenye mukhtasari juu ya kazi kuu mu Mathayo 28:18-20 na fahamu nyingine linganifu kwingineko mu bitabu bya injili, maandishi inasema

kuwa ili kutekeleza jukumu la Yesu, kanisa lazima lingekuwa “jamii ya mashahidi, . . . jamii ya kuabudu, . . . [na] jamii ya uanafunzi” (2, k. 6). Kote kote kwenye historia yake, maandishi inaendelea na kusema, kanisa limejihusiaha mu “kutangaza kwa neno na kwa vitendo habari njema ya Kristu, kusherehekea sakrementi, haswa Ekaristi, na kuunda pamoya jamii za Bakristo” (5, k. 7). Tena, “[y]ule Roho Mtakatifu anarutubisha na kupatia nguvu mwili wa Kristu kupitia kwa sauti hai ya injili yenye ilihubiriwa, kupitia kwa mawasiliano ya karibu ya sakramenti, haswa mu Ekaristia, na kupitia kazi za Mungu za huduma” (16, k. 11). Tukinukulu kutoka ku masomo mengine ya umoya wa madini, inahakikisha kuwa kanisa “linafichua Kristu ku duniya muzima kwa kuitangaza injili, kusherehekea sakramenti, . . . kunukuu kutoka ku masomo ya mapema ya umoya wa madini, kunahakikisha kuwa kanisa linafichua Kristu ku dunia muzima kwa kuitangaza injili, kwa kuisherehekea sakramenti, na kwa kuonyesha ule upya wa maisha uliyo tolewa na yeye hivyo kutazamia ufalme yenye ilipo tayari ndani yake” (58, k. 33). Na Mwisho ya maandishi (67, k. 39) inatangaza:

> Umoya wa mwili wa Kristu unahusisha zawadi ya *koinonia* au mawasiliano ya karibu yenye Mungu anapatia binadamu bote kwa neema. Kuna makubaliano inazidi kuwepo kuwa*koinonia*, kama mawasiliano ya karibu na Utatu Mtakatifu, umeonyeshwa mu njia tatu zenye hazihusiana: umoya wa imani, umoya wa maisha ya kisakramenti, na umoya mu huduma (mu mifumo yote yake hii, pamoya na kazi la Mungu na misheni).

Mu uchunguzi wake wa taswira ya kanisa kama batu ba Mungu, maandishi inaweza kuhusisha muundo huu wa utatu mu maisha na misheni ya kanisa kwa njia ya wazi wazi ku falsafa ya ofisi ya “mambo ya ku tatu” kwa Kristu, kama nabii, kuruhani, na mfalme: “Batu bote ba Mungu bameitwa kuwa batu ba kinabii, bakishuhudia neno la Mungu; batu benye ukuhani, benye banatoa sadaka mu maisha benye bali ishi Muuanafunzi; na batu benye kifalme, benye bana hudumu kama zana za uanzishwaji wa utawala wa Mungu.” Kwa kutilia mkazo, inaongezea: “Bamemba bote ba kanisa bako na mbinu hii” (19, k. 12).

Hii ingeonekana kutokuwa jambo muhimu ya wa mfanano ya kidini. Kyenye ina ulinganifu wa mafunzo ya Baraza la Pili la Vatican Mu *Mpango Kazi wake Mu Kitabu chake cha Mipango chenye kuzulumu juu ya*

*kanisa*yenye inafafanua baumini kama “baaminifu bote “all the faithful . . . kwa ubatizo bamekaribishwa mu Kristu, banahusisha batu ba Mungu, benye balifanywa kuwa bamiliki kwa njia yabo wenyewe mu ukuhani, unabii, na ufalme kwa mujibu wa ofisi ya Kristu na kuendeleza sehemu yabo ya kutelekeza misheni ya batu bote ba Kristu mu kanisa na ulimwengu.”[30] Mtazamo kama huo umechukuliwa mu masomo ya makanisa huru, na unaweza kupatikana mu idadi yenye inaongezeka ya karatasi za umoya wa madini. Kwa mfano, Tume ya Kimataifa juu ya Mazungumzo kati ya Bamethodiste-Bakatoliki inasema mu ripoti yake ya Brighton (2001): “Kwa sababu bafuasi ba Kristu bameekwa mu yake kupitiya ubatizo, bana tumikia pamoya mu ofisi yake ya kuhani, kinabii na kifahari, pamoya na mawasiliano ya karibu na kila mmoya wabo binafsi mu njia yake mwenyewe.”[31]

Kutoka kwenye Msimamo wa Methodiste Umoja, miunganisho hii inaweza kutelezwa sana, na kuongezea uelewa wetu wa maumbile na kuliita kanisa kama *koinonia*. John Wesley alisihi Bamethodiste ba mapeama kuweza kutangaza Kristu “mu ofisi zenu.”[32] Marejeleo ilikuwa yawe ni mpango wa mafundisho ya

[30] Mu*Baraza la Vatican la II: Karatasi Kumi na Sita za Kimsingi*, zenye zili haririwa na Austin Flannery, O.P. (Northport, New York: Costello Publishing Co., 1996), kk. 48-49.

[31] “Kuongela kwa Ukweli MuMapendo,” §§35-36, kumeweza kutajwa mu *Uwekaji pamoya: Pamoja kwa Utakatifu, Miaka Makumi ine ya Mazungumzo kati ya Methodiste na Katoliki*, ed. Michael E. Putney na Geoffrey Wainwright (n.p., [2010]), §73.

[32] Wesley anatangaza, “Sisi benyewe hatuko wazi nyuma ya Mungu, isipokuwa tunapomtangazia yote haya mu ofisi. Ili kuhubiri Kristu, kama mfanyia kazi asiyehitaji kuaibika, ni kumhubiri yeye, si tu kama Kuhani wetu mkuu, ‘mwenye alichukuliwa kati ya banaume, na kulapishwa na banaume, ku mambo yenye inahusu Mungu;’ kama vile, ‘kuturudisha na Mungu kwa damu yake,’ na ‘kuishi siku zote ili kuwa mwombezi wa bengine;’ — lakini vile vile kama nabii wa Bbana, ‘mwenye Mungu ameweza kutupa hekima,’ mwenye, kwa neno lake, na Roho Wake, ‘akituongoza Muukweli;’ — ndiyo, na kwa vile atabakia mfalme milele na milele; kwa kutoa sheria kwa bale benye amenunua na damu yake; kama rejesho kwa bale benye banafanana na picha ya Mungu benye alikuwa ametaja-awali mu mazungumzo yake; kama inatawala mu mioyo yote yenye ina amini mpaka pale kwenye anakuwa na mambo yenye ili finyiliwa na yenye ililetwa mu haki ya kudumu milele na milele,’(“Sheria yenye ilianzishwa kupitia kwa imani, Mazungumzo ya makini II,” *Mahubiri ya II*, yamehaririwa na Albert C. Outler, *Kazi za John Wesley*, juzuu la 2 (Nashville: Abingdon Press, 1985), kk. 37-38). Angalia sana kutoka ku “Kumbukumbu Kubwa” za 1745: “Q. 19. Ni mbinu gani bora ya jumla ya kuhubiri? A. Ili kualika, kushawishi, kusema juu ya Kristu, kuimarisha; na kufanya hivi mu mingi kipimo fulani mu kila ibada. Njia nzuri sana ya kuhubiri Kristu ni kuhubiri Yeye mu ofisi zake zote; na kutangaza sheria yake pamoya na injili yake, kwa baumini na bale bapagani.” Uchambuzi mfupi wa ziada wa ofisi hizo tatu (na haja yetu kwazo) unapatikana kwenye nakala ya Wesley juu ya Mathayo 1:16 mu *Nakala fafanuzi juu ya Agano Jipya.*

ofisi tatu (ao ofisi mara tatu, *munus triplex*) la Kristu, kama kuhani, nabii na mfalme. Mu maandiko ya Kiebrania, wajibu au kazi ya Masihi (Kristu, mwenye alichaguliwa) inaonyeswha mu njia tofauti, huku njia hizi tatu zikiwa zinaamuliwa kwa pamoya kuwa ndizo zenye zili jitokeza sana. Likiwa lilipatikana mu maandishi ya Bakristo ba mapema, wazo kuwa Yesu anatimiza wajibu wake tatu kwa pamoya linatokana na torati yetu ya Methodiste Umoja kwa njia moja kwa moja kutoka kwa Wesley (pamoya na theolojia ya kianglikana na John Calvin akisaidiana nabo) na kutoka kwenye Heidelberg Catechism (1563) yenye ilikuwa ni sehemu muhimu ya thorati ya kifalsafa ya Brethren wa Umoja wa Kiingilisti.

Ofisi hii ya fungutatu ilionekana kuwa na mvutio fulani ku Wesley, kwani ililingana na uelewa wake wa wokovu—juu ya kile tuliokolewa *kutoka* na kile tuliokolewa*mpaka*. Kama sisi tumejaaliwa “kuyua, kupenda, na kufurahia Muumba [wetu] milele mpaka milele,”[33] na kama hali yetu ya sasa ya kimatatizo—hali ya umaskini, kama Wesley vile anasema—sisi hatuwezi kuonyesha kwa usahihi ule uwezo wa maarifa, mapendo, na furaha, basi chenye tunahitaji si chochote kile ila uzalishaji upya wa uwezo huo. Tunahitaji kuachiliwa huru zidi ya kufungwa kwetu kwa kutojua, kukosa mapendo na kukosa matumaini (ao kutoka kwa utumwa wetu ku uongo na upotoshaji, zidi ya mapendo ya bongo na mwongozo na matumaini ya bongo). Tunahitaji kuzaliwa tena, na kupewa nguvu mu maisha mapya Mu“uhuru wa kitukufu wa batoto ba Mungu” (Warumi 8:21). Huu njo uwezekano wenye Kristu anatuletea sisi, na wenye Roho Mtakatifu anatoa kutoka kwetu sisi. Wesley bahubiri bake na batu bake kuendeleza maono hayo ya jumla mu akili yabo, na kutulia mpaka kwenye mahubiri ya wapunguzaji, “ofisi-moya” juu ya wokovu. Utambuzi wa*koinonia* wenye sisi tumeumbiwa, na wenye kanisa inafaa kupiga saini na kuhudumia, unahusu kuachiliwa huru zidi ya hali fulani (zitokanazo na nje na ndani) zenye zinatufanya sisi kukata tamaa, na kuingia mu mapatano ya maarifa, mapendo, na furaha na Ungu wa Utatu pamoya na uumbaji wote.

---

[33]John Wesley, “mwitikio ya Mungu juu ya Kazi Zake,” *Mahubiri ya II*, imehaririwa na Albert C. Outler, *Kazi za John Wesley*, kanda la 2 (Nashville: Abingdon Press, 1985), k. 397.

*Kuelekea Maono ya Pamoya* inatolea ushuhuda ku ukujaji wa pamoya kati ya makanisa mpaka kiwango cha kutangaza Kristo mu ofisi zake zote na kuwa na kuonyesha kuwa si kazi tu ya bahubiri. Ni kazi ya kanisa zima, mwito wa batu bote ba Mungu, bawe ni ba kibinafsi au ba kampuni; ni kazi la Mungu la jumla ku bakristo bote. Kwa sehemu ya, batu ba Methodiste Umoja bametambua hoja hii na ufafanuzi wake mu njia kazaa-kwa mfano, Mu kuhakikisha kuwa maonyehso muhimu na yenye ujenzi wa kitheolojia unahitaji vilevile kazi na uajibikaji wa kanisa mzima, kutekelezwa kwa upande wa kibinafsi na hata kijamii: “Kama Muungano wa Bamethodiste, tuna jukumu ya ushuhuda wa uaminifu wa Bakristu kwa Yesu Kristu, uhalisi wa matukiyo ku kiini ya maisha na ushuhuda wa Kanisa. Ili kutimiza jukumu hili, tunaangazia kwa makini juu ya urizi wetu wa kibibilia na kithiolojia na kulenga kuelezea kwa uaminifu ushuhuda yenye inatoa mu muda wetu binafsi.”[34]

Hata kama inatufahamisha na kuunda maisha na misheni ya batu bote ba Mungu—ao, pengine, *juu ya* inafanya hivyo—umbo hii ya mara tatu pia inatufahamisha na kuunda kazi la Mungu lenye lililapishwa. “[K]uanzia nyakati za mapema sana,” *Kuelekea Maono ya Pamoya* kinasema, “mingi baumini balichaguilwa kwa uongozi wa Roho na kupewa mamlaka kamili na uajibikaji. Bamchungaji benye balilapishwa ‘banakusanyika na kuujenga mwili wa Kristu kwa kutangaza na kufunza neno la Mungu kwa kusherehekea sakramenti na kuongoza maisha ya jamii mu kuabudu kwake, misheni yake na kazi lake la Mungu lenye linajali ’” (19, k. 12).[35]

---

[34] “Viwango vya Kifalsafa na kazi yetu ya Kithiolojia,” *Kitabu cha Mwenendo cha Kanisa Methodiste Umoja 2012* (Nashville: Matibaa ya Methodiste Umoja, 2012), kk. 79-80 (¶105).

[35] Utaoji wa ndani kwa ndani unatokea *Ubatizo, Ukaristi, na kazi la Mungu*, sehemu la kazi la Mungu, §13.

Kulingana na Kanisa Methodiste Umoja Mu mukutano wake wa kuunganisha mnamo 1968 iliweza kuitikia habari ya kazi la Mungu lenye lililapishwa lenye linaifafanua kama kazi la Mungu “maalum la Neno Sakramenti, na Mwenendo.”[36] Uundaji huu mpya, wenye hauonekani mu mambo ya rasmi juu ya kazi la Mungu lenye linalapishwa mu ama mazehebu yenye ilitangulia, iliweza kufikiria ushawishi wa mazungumzo ya mambo ya madini ya kisasa pamoya na kuanzisha umbo za idadi ya jamii nyingine za Bakristu. Habari hizi ziliwekwa wazi mu 1968*Kitabu cha Mwenendo* kinalinganga kwa ukaribu na kile chenye nimetoka kunukuu muda mfupi yenye ilipita *Kuelekea Maono ya Pamoya*:

> **Ulapishwaji** ni tambiko la kanisa lenye mingi banaaminiwa na mamlaka ya kuwa bamchungaji ba Neno, Sekramenti na Mwenendo:
>
> 1. Ili kulapishwa mu kazi ya Mungu la neno ni kumwitikioshwa, kuhubiri na kufunza neno la Mungu.
> 2. Ili kulapishwa mu kazi ya Mungu la Sakramenti ni kuweza kuwitikiwa na kutoa Sakramenti za Ubatizo na meza ya Bbana.
> 3. Ili kulapishwa ku kazi la Mungu la mwenendo ni kuitikishwa kuweza kubafnyaa balei ba kazi la Mungu, kuendeleza uangalizi wa kimchungaji, na kutoa Nizamu mu Kanisa. [37]

Inaafaa kusema kuwa umbo hii maarufu-yenye inatambulika ya utatu Mukazi la Mungu la kanisa ni kitu cha kipekee kutoka kile cha “kazi la Mungu mara tatu” la bashemasi benye bali lapishwa, mchungaji, baaskofu mu urizi wa kihistoria yenye inadaiwa na mingi jamii za Bakristu, na ile *BEM* yenye ilipendekezwa Mu kutiliwa maanani kwa umakinifu kwa makanisa yote mu kiu chao cha umoya wa kuonekana. Majibu ya

---

[36] *Kitabu cha Mwenendo 1968*, ¶302 (k. 107).

[37] *Kitabu cha Mwenendo 1968*, ¶309 (kk. 109-10).

kanisa ku *BEM* ilionyesha kuwa tuko mbali na kuya kokote kwa pamoja kwa wakati huu, na ndiyo maana huenda halitakuwa ni jambo la maarifa kuunganisha utambuzi wa pamoya wa bachungaji na makubaliano yoyote juu ya haya ao mpangilio wowote mwingine haswa juu ya ofisi ao mfumo wa kitawala wa kiuchungaji. Tunatazamia swala hili ndani ya*Kuelekea Maono ya Pamoya* yenye inatafakari hali hii. Mu *BEM*, “haja ya kuhakikisha” ilionekana kuwekwa mu makanisa yenye haifuata umbo la kazi la Mungu la utatu: bao “banahitaji kujiuliza benyewe kwa benyewe kama umbo ya utatu kama vile iliendelezwa haina madai yenye thabiti ili kukubalika na bao.”[38] Kwa mujibu wa majibu yenye ilipokelewa mu changamoto hii, Mu*Kuelekea Maono ya Pamoya* swali linaulizwa kwa usawa sana. “[S]isi tyenye inangozwa kwa kuyauliza makanisa kuweza kutimia kiwango na makubaliano kama kazi la Mungu la utatu ni sehemu ya mapenzi ya Mungu ya kanisa Mu utambuzi wake wa umoya kwa Mungu ao la” (47, k. 27).

Hii ni jambo ngumu, na lenye lina stahili kushugulikiwa sana mu sens ingine. Inaendelea kutafutizwa kwa umakinifu sana mu mazungumzo mseto ya umoya wa madini na mahusiano yenye batu ba Methodiste Umoya na bamemba bengine ba mila ya Bamethodiste na bale ba Wesley banahusika. Kuna makubaliano ya nguvu kati ya makanisa juu ya hoja muhimu zenye zinahusu mamlaka na uongozi mu kanisa, kwa mfano, kuwa makanisa yote kwa hakika yajumuishe muundo wao wa mingi toleo labo ku kazi la Mungu la uangalizi wa jumla (*episkopu*, kwa hakika “uangalizi” ao “usimamizi”), kuwa uongozi wote wa kiuchungaji mu kanisa unafaa kuendelezwa “kwa njia ya kibinafsi, ya kwa pamoya, na njia ya kusaidiana.”[39] Uchunguzi zaidi wa tabia ya uongozi mu kanisa unaweza kusababisha maelewa mazuri ya muundo wake, yenye haijafikiriwa sasa.

Mu Kanisa Methodiste Umoja, hata kama tyenye ina bashemasi, bazee (balei), na baaskofu, hatuna “kazi la Mungu la Utatu” kwa maana ya kuwa ile istilahi yenye inatumika mu tamaduni nyingine ao mazungumzo mengine ya mambo ya madini. Tunalapisha bashemasi na bazee; hatulapishi baaskofu

---

[38] *BEM*, Sehemu ya kazi la Mungu, §25 (k. 25).

[39] *BEM*, sehemu la kazi la Mungu, §26 (kk. 25-26). Lugha inatiliwa mkazo mu *Kuelekea Maono ya Pamoya*, 52 (k. 29).

benye bamechaguliwa kutoka kati ya bazee ili kuweza kutekeleza wajibu maalum wa uangailzi.[40] Aiza, kwa sasa hatuendelezi ulapishwaji wa, “hatua kwa hatua,” wenye mtu wa kulapishwa kama muzee lazima kwanza alapishwe kama shemasi. Mu myaka ya mapema ya Kanisa Methodiste Umoja, yani Kanisa Methodiste Umoja mpaka kwa muungano, ulapishwaji wa hatua kwa hatua ndio yenye ilizoeleka: bashemasi benye bali lapishwa ni kipengele kilicho eleweka kama hatua moja mbele juu ya ulapishwaji kama bazee, na kuingiliana kwa umbali na uanachama wa uangalizi wa moya Mu mukutano wa mwaka. Mzee alipewa “mamlaka kamilifu ku kazi la Mungu la Neno, Sakramenti, na Mwenendo,”[41] na kuliukwa na uundaji wa kando yenye ilikuwa sambamba na kazi la Mungu la Shemasi, jambo lenye lilionekana muhimu sana kama lile litatuhusisha mamlaka ndogo ya kushiriki mu shughuli kama hizi.

Wazo la “shemasi wa kudumu,” yani, bashemasi benye bata lapishwa mu ofisi hiyo si kama kiwango mu njia ya ulapishaji kama bazee lakini kwa mwenendo wa kuendeleza kazi ya Mungu ya mara kwa mara yenye inajitokeza kama bashemasi, ilikuwa ikizidi kupata umaarufu mu idadi kazaa za makanisa tayari kwa wakati huo Kanisa la Methodiste Umoja likaumbwa. (“Shemasi wa kudumu” na “shemasi wa mpito,” hata kama ni maneno maarufu mu mazungumzo haya, ni ya kuchanganya kiufundi, juu ni umbo ya ulapishwaji wa hatua kwa hatua wa bazee benye hauwasitishi kuwa bashemasi.) Bashemasi wa kudumu benye bali wazi kuoa pamoja na banaume wenye habayaowa (lakini kama ukuhani, ni wazi tu kwa banaume) uliitikishwa na Baraza la pili la Vatican na kutangulizwa mu sehemu tofauti za kanisa la Katoliki la Urumi mu kipindi cha myaka kumi yenye ilifuata. Ushirika wa Baanglikani na baraza ya makanisa ilisiimarisha ushemasi ao “muito” wakati moya. Nyuma ya idadi kazaa ya majaribio kwa miaka (ikiwemo ofisi yenye silapishwi ya mchungaji wa Kishemasi), Kanisa Methodiste Umoja lilianzisha shemasi wa kudumu mwenye alilapishwa mu 1996, na wakati huo likapuzilia mbali mwenendo wa hatua kwa hatua. Mu kanuni yetu ya sasa, bashemasi benye bana taka kuwa shemasi na bazee benye banataka kuwa bazee bako ku fasi “tofauti,” na lugha yenye inaonyesha tabia la kazi la Mungu yenye kila moyawapo amelapishwa—kwa upande wa shemasi, kazi la Mungu la “Neno,

---

[40] *Kitabu cha Mwenendo 2012*, ¶402 (k. 315).

[41] *Kitabu cha Mwenendo 1968*, ¶313 (k. 110).

Huduma, Haki, na Rehma," na kwa upande wa muzee, kazi la Mungu la "Neno, Sakramenti, Mwenendo na Huduma"—byote hibi binenuiwa kuonyesha kuwa hata kama huenda kukawa na sehemu fulani za pamoya juu ya uajibikaji kunazo pia sehemu tofauti na maalum mu kila sehemu yenye yule mwingine hatuambii.[42]

Juu muundo huu wa uwekaji mwenendo wa kazi la Mungu ni mupya kwa kiasi fulani—kama ugunduzi wa kusindikiza yenye ilianzisha "Mwenendo" wa Bashemasi na "Mwenendo" wa Bazee kama mashirika ya chuo yenye ilitunga bale bote benye balilapishwa mu ofisi zabo husika—namna mapangilio haya yatakuwepo kwa kadiri muda vile unasonga ni jambo lenye tunazidi kungoya kuona. Picha ni ngumu kueleweka kutokana na hoja kuwa Umethodiste Umoja pia unaangazia idadi fulani ya ofisi za kimchungaji zenye zinatambuliwa na wajibu wenye hauhitaji ulapishwaji, ba mingi banaweza kuwa bamehusika mu shughuli kuu kwa kawaida zenye zina husiana na ofisi za ulapishwaji—hali yenye ina zua mshangao mkubwa kutoka ndani na hata sana ya kanisa.[43] Tafakari sana juu ya mazungumzo ya mambo ya madini, na ushauriano yenye inaendelea kwa mseto mpana wa bia wa umoya wa madini, utakuwa muhimu kwa maendeleo yote ya kuwajibikia juu ya maswala haya yenye inaonekana hayaishi. Tunayo maono makuu na ushuhuda kutoka ku uzoefu wetu sisi wenyewe wenye tutatoa mu mudahalo wa umoya wa madini, kama yala yenye inatokana na kuwa tayari kwetu kuitikia hali mpya na kujitolea kwetu kwenye uthabiti na kusikobadilishwa mpaka kwenye kushiriki kikamilifu kwa banamke mu uongozi wa kichungaji kwa mifumo yake yote. Lakini hapawezi kuwa na shaka kuwa pia tunayo mambo ya kujifunza kutoka kwenye uzoefu wa batu bengine. Tunaweza kupata kati ya mambo mengine kuwa uthibitishwaji tena na uchunguzi wa umbo wa utatu ya "Neno, Sakarementi, na Mwenendo" Mu maendeleo ya theolojia yenye ujenzi na kamilifu sana mu kazi la Mungu itakuwa na manufaa ya mambo ya madini na vile vile maisha ya jamii yetu sisi binafsi.

---

[42] *Kitabu cha Mwenendo 2012,* ¶¶329.1, 332. Ni kwa njia bora vipi njo uundaji wa maneneo yenye inaonyesha utofauti wa kuulizwa swali.

[43] Juu ya mada haya yote, tazama *Kitabu cha Mwenendo cha 2012*, ¶¶266-370, John E. Harnish, *Mwenendo wa Kazi la Mungu mu Kanisa Methodiste Umoja* (Nashville: Abingdon Press, 2000), na Thomas Edward Frank, *Kanuni, Mienendo, na Misheni ya Kanisa Methodiste Umoja* (Nashville: Abingdon Press, 2006), chapter 7.

## III. Maono na Mienendo

Mu sehemu hii ya kuitimisha, tunachukua Mu utiliaji maanani wa moja kwa moja maswali matatu yenye ilizuiliwa mu kurasa zetu za ufunguzi na tumekuwa tukiandamana nayo kwa angaa kitabu kizima tulipoendelea.

Kwanza, tunawezaje kupatia sifa za uhusika wajibu fulani wa Kanisa Methodiste Umoja Mu“Kanisa la Duniya Muzima”? Ni nini kiwango chetu mu ekolojia ya mwanzo? Pili, ni maono yapi yatakayo weza kuzuiliwa mu kushiriki kwetu mu mazungumzo ya mambo ya madini ili kutusaidia kushughulikia sana kwa njia bora na ya kikamilifu pamoya na maswala tata yenye inazungukia “mseto wa halali”, byote kwa juu vinaathiri maisha yetu binafsi na misheni mu Kanisa Methodiste Umoja na mu mahusiano yetu yenye inaendelea na jamii nyingine za Bakristu? Tatu, ni vipi vile maono yetu yenye nguvu mpya ya mambo ya kanisa vile ita kutufahamisha maazimio yetu juu ya kanuni yetu—yaani, namuna vyenye tunaunda maisha yetu ya pamoya mu huduma ya misheni yetu?

### <u>Umethodiste Umoya na Kanisa la Duniya Muzima</u>

Kunazo hatari mu jaribio lolote la kujiweka Mu uhusiano na makanisa mengine, au kufafanua umaalumu wetu sisi binafsi. Tunaweza kuzidisha makadirio yetu ya umaalum, haswa kama tutachukulia sifa kubwa kama zenye umuhimu au uzuri. Tunaweza kuzidisha makadirio yetu Mu kiwango chenye sifa kubwa ze tunalomba na kwa hakika zenye zinaweza kupatikana miongoni mwetu. Picha tuko nayo juu yetu sipeke inaweza kuwa na ufananisho mdogo sana juu ya kile kyenye bengine banaweza kutuambia kutuhusu sisi wenyewe. “Ili kujiona kama bengine banavyo tuona sisi,” H. Richard Niebuhr alisema, “ao kuwafanya batu bengine kuwasiliana nasi kutokana na kile kye banaona bakiangalia maisha yetu kutoka inje ni kuweza kuwa na hali ya uzoefu ya kimaadili.”[44] Kwa hatari ya kuaminika, basi, tutapendekeza vipengele vikuu vitatu, kati ya

[44] H. Richard Niebuhr, *Maana ya Ufunuo* (New York: Macmillan, 1960), k. 62.

vingi vyenye vinaweza kutajwa, vyenye vinaweza kuwa alama za utambulisho wa methodiste umoja.[45] Hizi ni, kwa kiwango kidogo sana, sifa za kuhemsha: mambo yenye—kuhukumu kutokana na umuhimu tyenye inazipatia sifa hizo kwa kufuata kanuni—tungependa kujulikana kwani alama kiri zenye tulikuwa tujulikane nazo. Ni alama zenye tunakiri kuwa tunaamini. Hata kama zote tatu bila shaka zimekita mizizi mu urizi yetu ya pamoya na jamii zetu za Wesley na Methodiste—yani, mu mambo ya kujitolea kwa njia maalum ya torati hii yenye ilitajwa mwanzo wa karatasi hii—inawakilisha tabia ya Umethodiste Umoja kama mfumo na maonyesho fulani ya mambo ya makanisa juu ya torati ya pamoya. Kujitokeza kwake mu mazungumzo ya makini ya Methodiste Umoja kunayafanya kuwa sehemu nzuri ya kuanzia juu ya kufikiria kwetu.

Moya ya sifa hizi lazima iwe kuhusiana na *upana wa neema*, mitazamo mbili. Mitazamo hii inalingana, kwa njia fulani, huku mitazamo ya kwanza ya yale mambo matatu maalum ya kujitolea juu ya torati yetu. Mtazamo wa kwanza ni kujitolea ku Wesley—haihusu kwa vyovyote vile batu ba Wesley, bila shaka inadaiwa na mila hii—kuwa mapendo ya Mungu inarefushwa kwa kwa viumbe vya vya Mungu na si tu kwa bamoyamoya. Mustari kutoka ku 1Timotheo 2:4 wenye tulitaja zamani unaweza kuwa kauli mbiyu Methodiste ya Umoja: Mungu alifichua Mukristo "anatamani kila mtu kuokolewa na kufikia kuyua maarifa ya ukweli." Neema ya Mungu inapatikana kwa batu bote, kwa kiwango sawa. Miongoni mwa mambo mengine, hii inahusisha utiliaji mkazo yenye iliwekewa kanisa la Methodiste Umoja juu ya ujumuishaji kamili mu memba na kazi la Mungu, ili kanisa liweze kuwa ishara yenye uaminifu wa upana wa neema ya Mungu. Sina haja ya kusema, mienendo yetu wakati mwingine mmepungukiwa na maazimio ya Mungu.

Mtazamo wa pili wenye upana wa neema ni mada maalum lazima uwe unahusu kile kiwango ao ufikivu, lakini ikiwa na nia ao atari yake. Ni uhakika kuwa wakati neema ya Mungu inapokelewa mu uhuru wenye unamuunda, inabadilisha. Ina ongoza, kama Wesley vile alisema, "ku mabadiliko halisi" mu ya yule mpokeaji. "Kama yeyote yumo Mu kristo, yeye ni kiumbe kipya" (2 Wak. 5:17). Kuzaliwa upya, kupokea imani "kujazwa na nguvu za mapendo" (kama Wesley angesema mu Wagalatia 5:6), kuwa na "mapendo ya

---

[45] Kwa kushughulikiwa kuzuri na kumakinika kwa vipengele vya sifa vya mila ya Methodiste kwa ujumla sana, kuhusiana na njia ya kufikiria ya "nakala nne" ya taarifa ya imani ya Nicene see Russell E. Richey (na Dennis M. Campbell na William B. Lawrence), *Alama za Umethodiste: Theolojia mu Mienendo ya Mambo ya Kanisa* (Nashville: Abingdon Press, 2005).

Mungu . . . ikiwa ime muagiwa mu moyo yetu kupitiya kwa Roho Mutakatifu" (Waarumi 5:5)—haba balikuwa ba Methodiste ba mapema, na bamekuwa batu ba ukoo abo ba kiroho, benye uhalisia halisi wa mambo benye bali pitia na kuishia ku atari mpya za kibinafsi na kijamii kama vile mapendo hayo kuingiliwa mu mambo ya kibinafsi yenye upya na kuonyeshwa si tu kwa mashahidi ya moja kwa moja na ya wazi wazi juu ya injili lakini pia mu shughuli mu imarishaji jamii (*koinonia* tunaweza) njia kuu mbali mbali kuanzia mahusiano binafsi mpaka kwenye uanzishaji wa hospitali mpaka vyuo vikuu, kuanzia mu kaza Mungu za ufikivu wa baumini ba mu mpaka mu kushiriki ngufu za bafasi-kubwa juu ya utengezwaji wa kijamii na marekebisho. Nguvu za kazi mu torati ya Methodiste mu Umoja kama ilivyo tajwa, kwa mu fano, mu bifungo bingi bia kanuni za kijamii na maazimio ya mara kwa mara mu mukutano mukuu ni kuunda talaasisi na mienendo yenye (kwa uamusi wetu finyu nayenye inakubalika ku muda wowote fulani) kuimarisha hali-njema ya ku binadamu, na kupatia changamoto pale benye haba husiki.

Moyawapo ya maelezo mafupi binafsi ya John Wesley juu ya upana wa neema ya Mungu mutazamo huu wa pili aliandika:

> Kwa uokovu ninamaanisha, si tu (kulingana na fikira ile mbaya) ukombozi kutoka jahanamu, ao kwenda mbinguni; lakini ukombozi wa sasa zidi ya zambi, urejeshi wa nafsi mpaka ku afya yake ya mwanzo, usafi wa asilia; ufufuzi wa maumbile ya kiungu; upatiaji upya wa nafsi zetu nyuma ya mfano wa Mungu mu muhaki na utakatifu wa kweli, mu haki rehema na mu kweli. Hii inamaanisha mitazamo yote takatifu na ya mbinguni, kwa atari yake na utaratibu wake wa mazungumzo.[46]

Umethodiste Umoja unashabaha kukumbatia upana muzima juu ya wasi wasi huu. Wakati mwingine utakasaji wa mu kwa mu na upatiaji upya wa moyo unatiliwa mkazo, na wakati mwingine ni ngufu za kufanyia kazi kitu

---

[46] John Wesley, *Baba mwenye Kivutio Banaume ba Sababu na Dini, Sehemu I* (1745), mu *vivutio Banaume ba Sababu na Dini, na Barua Fulani Wazi Zenye zinahusiana*, haririwa Gerald R. Cragg, *Kazi za ya John Wesley*, kanda 11 (Oxford: Oxford University Press, 1976), k. 106. "Mazungumzo" muda wa Wesley na matumizi ilimaanisha kitu kama "utangamano wa kijamii," mwenendo wa mtu kuelekea na ku mahusiano kwa batu bengine.

chenye batu bame chukulia kuwa mufafanuzi wa mapana sana “utakatifu ma mazungumzo”—uimarisha wa “haki, rehema, na ukweli” kote kote mu mwenendo wa kijamii—wenye unapokea utiliaji maanani sana. Tofauti kama hizo za utiliaji mkazo zinafaa wakati zinaelekezwa ku mahitaji fulani zenye tunajipata mu sisi wenyewe. Lakini tunakuwa mu hali muzuri sana wakati tunatambua uhusiano wa karibu na bitu hibyo biwili na mu jambo lenye linapungua hali yetu muzuri sana wakati tuna bigonganisha bitu hibyo moja kwa nyingine.

Alama ya pili ya utambulisho wa Methodiste Umoja—yenye ina husiana na jambo la tatu maalum la kujitolea juu ya torati yetu, kushughulikia nia ya uundaji wa jamii wa mapendo ya Mungu—linaitwa “*upatanisho kufanya kazi moja*.” “Utiifu” ni neno lenye linahusiana na (hata kama si kisawe) mu mazungumzo ya mambo ya kanisa na hali nyingine za kushughulikia mambo ya kanisa na hali nyingine za kushughulikia mada ya mwenendo na mamlaka mu *Kuelekea Maono ya Pamoya* kutilia maanani mambo yenye sisi batu ba Methodiste Umoja banaweza kushurikiana na kuwa mumoja. Kazi letu la Mungu “mpangilio”, ukuu (baaskofu na basimamizi ba wilaya), na mfumo ba makutano byote binanuiwa kuwa hali za kuwa muumoja. Hibi byote bitatu binataka kuimarisha maadili na mienendo ya msaada wa bamoya na uwajibikaji wa bamoya, wa uwangalizi wa kuchangizwa (hapa, ni muhimu kukumbuka kuwa mtazamo mumoya *wa askofu* yenye ilitaywa mu *Kuelekea Maoni ya Pamoya* ni “uratibu”), na wa kupatia nguvu bitu byote zawadi kati ya zote. Siku zote ni swali wazi juu ni vipi vienye miundo yetu ya sasa ilivyo miema, na kanuni kuu kuhudumia uhusiano wa kuwa mumoja na njia ya kufanyia kazi yenye tunatafuta, na kila mojawapo ya mambo matatu yenye ili taywa hivi punde yenye sasa ina fanyiwa uchunguzi mwingi kwa hayo. Kanuni muhimu, hata hivyo, inatuunganisha sisi na bamoya bamoya maono ya kina sana ya nila ya kale ya Bakristo kuhusiana na uhusiano wa mawasiliano ya karibu mu na kati ya jamii za Bakristo.

Mazungumzo munaendelea mu kanisa letu juu ya umbo na maonyesho bora ya muundo wa kuwa mumoja na kanuni mara nyingi byote binafutiliwa mbali kwa kuonekana kuwa shughuli zisizo faa mu mambo za kisiasa na uchezaji wa karata ya nguvu. Huku mara nyingi byote hibi bikiwa sawa, upingaji kama huu unazuia mapambano wa kina sana. Kama, ilivyotajwa mapema, kuwa mumoja na misheni byote bimeunganika mu kwa mu, na mu kilicho kizuri sana mu mijadala hii si chochote kile zile nguvu za muundo wetu wa kuwa mumoja yenye inajitokeza sana mu kanisa kama chombo cha kyenye kinaazimia kuwa mu dunia nzima.

Alama ya tatu ya utambulisho wa UmethodisteUmoja yenye itatolewa inao uhusiano wa karibu na zile za kwanza mbili, na inaweza kuonekana kuwa fafanuzi wa hizo zote. Ni kujitolea kwa *onyesho la theolojia* kama kazi ya kanisa nzima. Uwepo mu ya *Kitabu cha Mwenendo* si tu mu viwango tu za msimamo wa mafundisho, lakini pia ku taarifa juu ya "kazi yetu ya ki theolojia," yaonyeshaa umuhimu wa kujitolea huku. Kumbuka kuwa onyesho la kitheolojia *halisawazishi* viwango tuna hitaji na tunahakikisha byote.

> Kazi ya ki thiolojia, hata kama inahusiana na maonyesho ya msimamo wa mafundisho ya kanisa, inahudumu kazi tofauti. Uhakikisho wetu wa ki msimamo wa mafundisho mu utambuzi wa ukweli wa Bakristo mu mawazo yenye ina badilika-siku zote. Kazi yetu ya kithiolojia inajumuisha upimaji, upatiaji upya, ufafanuzi, na matumizi na mitazamo yetu ya kimsimamo wa mafundisho mu utekelezaji wa mwito wetu "kueneza utakatifu wa maandiko kote kote mu fasi hizi."[47]

Kwa tabia na yenye ilimo yabo binafsi, viwango byetu bya msimamo wa mafundisho habiruhusu lakini pia bina hitaji uwajibikaji ule, uhusishwaji muhimu wa fikira wenye "Kazi Yetu ya Kithiolojia" inafafanua. Kazi yetu ya kithiolojia lazima iwe "ya kupinga na pia ya kujenga," "byote biwe bya kibinafsi na bya kwa pamoya," "biwe bya mukutaza na bya roho kuwa mwili," na "muhimu sana bya kimatendo."[48] Ili kuweza kupewa umakinifu na uhakikisho wa kazi ya kithiolojia ya kanisa yenye inaendelea ni kilele cha kweli cha kanisa Methodiste Umoja. Itatuweka muhali muzuri wakati tuna tafuta kuwa mfano halisi wa agano letu la kuwa mumoja na ubunifu wa kithiolojia, unyumbukaji, na ubora mu mikitaza mipana yenye inaongeza mu duniya muzima. Kama ilivyo kwa sifa za kwanza mbili zenye zili tajwa ni eneo lenye kujitolea kwetu kwenyu kanuni kuna hudumu kwa mfano wa kuhukumu na kuongoza mienendo yetu.

## Mseto na mzozo

[47] *Kitabu Cha Mwenendo 2012*, ¶105 (k. 78).

[48] *Kitabu cha Mwenendo 2012*, ¶105 (kk. 79-80).

Sifa hizi tatu zikiwekwa kwa pamoya, na kuongezewa hekima ya mambo ya kanisa zina weza kuelekeza ku njia ya kuangazia ugumu wetu wa sasa zidi ya mzozo mu kanisa.

Inafaa kusemekana kuwa, tatizo letu si mzozo. Tatizo letu ni muna sisi njia nyingine tunashughulikia mzozo. Tunge fanya vema kama tungekumbuka kama mzozo ni "mu" kanisa. Unatarajiwa. Kutoelewana kunakounda mzozo kunaweza kutokana na (kama nitatumia lugha ya Wesley) "nini cha kufunya, namuna ya kufunza."[49] Ikiwa imepachikwa mu ya na ikiandamana na kuto elewana huku kunaweza kuwa ugumu mwingine, wakati mwingine ukiwa umejificha ao hujatambulika, wenye pia una sababisha wasi wasi: uadui yenye inatokana na historia ngumu na mahusiana na batu na bikundi binavyo husika na utofauti wa maadili ya kisiasa ao ya kitamaduni, mapambano zidi ya kumiliki na matumizi ya nguvu na kazalika. Vianzo tofauti na miseto ya Mizozo byote binaweza kuhusiana mu kwa mu mufano wowote ule. Tukiangalia museto wa matumizi ya binadamu mu kanisa, wakati mwingine inafanyika kuuwa mzozo juu ya suala moya unaimarishwa ao unatumiwa bibaya na batu binafsi kukamilisha pamoya pamoya nia nyingine ao kutosheleza mahitaji mengine. Mzozo ni mgumu kama vile yenye ilivyo maarufu.[50]

---

[49]Fomula ya mara kwa mara-yenye inanukuliwa inatokana na ajenda za mukutano wa kwanza wa Methodiste mu London muunamo 1744: "Nyuma ya pamoya pamoya muda yenye ili tumika mu maombi, muundo wa mukutano wenye ulipendekezwa, wenye kurejelea: (1) Ni nini cha kufunza, (2) Namuna ya kufunza, na (3) Ni nini cha kufanya, namuna ya kuhakikisha msimamo wa mafundisho yetu, nizamu, na mienendo." (Kutoka kutoleo la kwanza la Wesley lenye lilichapishwa juu ya kumbukumbu, lenye tarehe 1749, mu *Vyama Bya Methodiste: Kumbukumbu za Mukutano wa*, haririwa na Henry D. Rack, *Kazi za John Wesley*, kanda la 10 [Nashville: Abingdon Press, 2011], k. 778.)

[50]Mafasirio mfupi wenye mzozo ni huu yenye ili tolewa na Kituo cha Kidenishi juu ya Kusuluisha Mizozo: "Mizozo ni kutoelewana kunako sababisha wasi wasi mu ya na kati ya, batu." Bjarne Vestergaard, Erik Helvard and Aase Rieck Sørensen, *Usuluhishaji wa Mizozo—Kufanya Kazi na Mizozo* (Frederiksberg, Denmark: Kituo cha Kidanois Cha Kusuluhishia Mizozo, 2010), k. 1, kinapatikana ku http://lnu.se/polopoly_fs/1.105781!2011%20DCCR_BASIC%20MATERIAL.pdf.

Kanisa bila mzozo lina uwezekano mkubwa sana wa kuwa kanisa lenye linashindwa kuwa kanisa. Kumbukuka kuwa ni Mungu mwenye ana tuleta mu kanisa ao mwenye analeta kanisa kwetu sisi, kuliunda kanisa kuwa kati kati yetu kwa nguvu za Roho Mutakatifu. Tunaletwa pamoya mufano kwanza kwa neema, si kwa sababu tunachangiza maono sawa, desturi, mienendo ya kitamaduni, ao hata maadili ya kijamii. (Tena, tilia maanani matumizi ya binadamu mu kanisa, tunaweza kusema kuwa mpaka kiwango chenye tumekuya pamoya *juu ya* tunachangiza maono sawa, maadili, msimamo wa kijamii na kazalika huenda tusitambue zawadi kubwa sana ya *koinonia* mu Roho.)  Kupitia yale tyenye una pitia na batu bengine mu jamii Bakristo, tunaweza bila shaka kuja kuchangihali kiasi kizuri cha mambo haya kwa utaratibu. Akili zinaweza kubadilisha—pengine kwa nguvu sana wakati si mfano wa muhusika mumoya kushinda mabishano zidi ya batu bengine lakini pahari pake abo kuweza kuongozwa kupitia kwa uzoefu kwa pamoya mpaka mu uelewa mukubwa sana kuliko yeyote yule aliye husika zamani. Tunaweza kugundua ao kukubaliana juu ya mambo mbali mbali. Lakini kushinda ao kufuta utofauti si hasa matokeo mazuri sana. Utofauti mwingi ni sehemu ya mseto mzuri wa uumbaji, mseto wenye ni “zawadi kutoka ku Bwana” unafaa kuheshimiwa vile vile.

Vile vile, utofauti mwengine mu ya kanisa husaidia kanisa mu misheni yake ya duniya yenye mseto. Kwa sasa, makanisa inakabiliwa na hali zenye hayajakabiliwa tena mbele. Teknolojia mpya zina leta uwezekano wenye haukufikiwa zamani; maarifa mapya inabadilisha uelewa wetu juu ya sisi benyewe, na dunia yenye tunaishi mu. Wakati kanisa linakabiliwa na hali mpya na linatafakari juu ya jibu muzuri sana, ni vyema kuwa na mseto mpana sana wa uzoefu karibu nasi. Ili kuelewa na kuheshimu utofauti wa kila mumoya wetu na njia zenye zote tunachangia mu kutimiza misheni ya kanisa ni njia mojawapo ya kuchangia na kitu kama ruwaza ya umoya wa madini ya “kuya pamoya,” kwa torati zinashikiliwa kati ya umoya wa kina sana na wenye nguvu sana,-ni uzoefu yenye inatumainiwa kati ya ba memba ba baumini ba ndani ya ao mfumo mwingine wa *eklesia* vile vile.

Mu mifano kama hiyo, utofauti hautishii umoya wenye Mungu alitaka pahari pake unauzidisha. Wakati huo, pamoya pamoya, mugogoro unaanzishwa kwa majibu tofauti kwa maendeleo haya kama tulivyo ku "kulenga kuonyesha kwa uaminifu ushuhuda tyenye ina toa kwa nafasi yetu sisi wenyewe." kuna mifano ya mugogoro ynye batu tofauti wana uamuzi usioingiliana ao pinzani juu ya pamoya pamoya swala lenye wanaona ni muhimu ku tambulisha kwa kanisa na misheni lenye uamuzi wake yenye inanekana kuwa sana ya uwezo wetu. Wakati mugogoro unaweza kusuluhishwa kupitiya mazungumuzo ao majadiliano, kupitiya hatuwa yenye batu bote banao husika wanoshughulikia kwa heshima hafla nzima inaweza kuwa ushuhuda wenye nguvu kuhusu injili. Kama kanisa sisi sote hatuja itwa kuepuka mugogoro ao kuufu tilia mbali, pahari pake tumeitwa kuushughulikia kwa ukombozi.

Wakati usuluhishi haonekani kuwa unawezekana machaguo yetu ni yepi?

Taarifa ya mapema sana ya mambo ya kanisa ikitufahamisha uelewa yenye ili onyeshwa mu *Kuelekea Maono Pamoya*, unahakikisha: "Kusudio la kanisa ni kuwaweka batu pamoya na Kristu mu nguvu za Roho, ili kuonyesha mawasiliano ya karibu mu maombi na hatuwa hivyo basi kuelekeza mu ukamilifu wa mawasiliano ya Mungu, ubinadamu, na uumbaji mzima mu utukufu mu ufalme."[51] Pengine mambo haya hatufai kusonga kwa haraka sana kuelekea mu suluhisho la kidemokrasia juu ya utofauti wetu wa mu sana, hata hiyo ikieleweka sana kwa batu bote.

Jambo muhimu la kutilia maanani muunganisho huu ni kuwa huenda tusiwe mu hali ya kushughulikia uamuzi wa kuwajibika juu ya suala la sasa. Huenda tusijue yote tunahitaji kuyuwa. Huenda tusiwe na mali ya kutosha mu hali. Huenda tusiwe na ukomavu wa kirohoo wa kulola kile tunacho hitaji kulola. Huenda hata hatukuuliza maulizo yetu kwa njia ya usahihi.

---

[51] "Umoya wa Kanisa kama Koinonia, Zawadi na Mwito," Kusanyiko la Saba la Baraza mu Kanisa mu Duniyani, Canberra, 1991, mu *Kikundi cha Mambo ya Kanisa: Mkusanyiko wa Maandishi Muhimu na Sauti*, umehaririwa na Michael Kinnamon na Brian E. Cope (Grand Rapids, Michigan: Wm. B. Eerdmans, 1996), k. 124.

Huenda, kwa ufupi, tukahitaji kufaidi pamoya pamoya unyenyekevu wa kiakili na kihisia, a kushughulikia pamoya pamoya, tabia yenye itaruhusu hekima kukua.

Sifa za torato yetu ya Methodiste Umoja huenda ikatuhimiza kufikiria uwezekano huu. Mahubiri ya John Wesley, "Hali ya Kikatholiki," tunapata utambuzi huu wazi:

> Ni atari haiwezi kuepukika na uzaifu na ufupi wa uelewa wa binadamu wa sasa wenye banaume mbali mbali batakuwa mu akili mbali mbali, mu dini pamoya na mu maisha ya umma. Kwa hiyo imekuwa tangia mwanzo wa duniya na kwa hiyo itakuwa hivyo 'mpaka urejeshi wa biumbe byoye.'
>
> Na vile: hata kama kila binadamu anaamini kwa vyovyote vile kuwa kila maoni fulani yenye yeye anashikilia ni kweli (ili kuamini maoni yoyote si kweli ni jambo lile lile kama kuto-yashikilia maoni hayo) wala hakuna binadamu banaweza kuhakikisha kuwa maoni yote binafsi yakiwekwa pamoja ni ya kweli. Apana, kila binadamu mwenye kufikiria anahakiki-shiwa kuwa yeye haoni *humanum est errare et nescire*—ili kutoyuwa bitu bingi na kukoseya pamoya pamoya, ni hali yenye inahitajika ku binadamu. Hii hivyo basi, yeye ni mwenye akili mambo yake binafsi. Yeye anayuwa mu mambo hii yote kwa jumla kuwa yeye mwenyewe amekosea; hata kama mu mambo fulani amekosea hayuwi, ao pengine hawezi kuyuwa.[52]

Tunaweza kuwa na hakika kuwa tumekosea mu pamoya pamoya ya kile kyenye kinafikiria tunayuwa. Ni mchango gani ndo ufahamu huu unaweza kufanya mtazamo wetu wa hali ile kuwa mu mugogoro?

Ufahamu mwingine kutoka ku maandishi ya John Wesley unatupa maono sana juu ya hali hii. Utangulizi wa "mahubiri ya wastani":

---

[52] John Wesley, "Hali ya Kikatholiki," *Mahubiri ya II*, imehaririwa na Albert C. Outler, *Kazi ya John Wesley*, kanda 2 (Nashville: Abingdon Press, 1985), kk. 83-84.

9. Unashawishiwa kuwa yenye inana kwa uwazi sana kuliko mimi? Hakuna uwezekano kuwa utaweza kufanya hivyo. Basi nichukulia mimi kama vile utakavyotamani kushughulikiwa wewe mwenye kutokeya mabadiliko ya hali. Nielekezee njia muzuri sana kuliko ile nilio wahi kuyuwa. Nionyeshe mimi jambo hilo Kutokana na ushuhuda wazi ya Maandiko. Na kama nitapotea potea ku njia yenye nimezoea kupitia, na kwahio nataka kuondoka, ng'ang'ana na pambana na mimi kidogo, nishikilie mkono, na uniongoze mimi mpaka pale ninapoweza kuongozwa. Lakini usikasirike kama nitakuomba kuto nipiga ili kuharakisha hatua yangu. Ninaweza kuenda lakini kwa unyonge na upole kwa njia muzuri sana —kisha, sitaweza kuenda kamwe. Wacha nisikulombe wewe, sana, kutonipatia majina magumu ili kunifanya kupitia njia sahihi? Hebu tuseme siku zote ningekuwa nafanya mambo mabaya nashuku kama haya itanifanya kuwa sahihi. Pahari pake itanifanya kuenda mbali sana na wewe—na hivyo kupote sana na sana.

10. Apana, pengine wewe kama una kisirani, namiye pia nitakuwa na kisirani, na kutakuwa na matumaini madogo ya kutafuta ukweli. Kama pindi kisirani itapanda, *eute kapnos* (kama vile Homer mahali fulani vyenye ana onyeshea), moshi huu utajaa kwenye macho ya nafsi yangu kuwa sitaweza kuona vizuri. Kwa minajili ya Mungu, kama itawezekana kuepuka hebu na tusichocheane benyewe kwa benyewe juu ya kisirani. Hebu na tusiwashiane benyewe kwa benyewe moto huu wa jihenamu na isitoshe kuupuliza ili ukaongezeke. Kama tungeweza kutambua ukweli kutokana na ule mwanga mubaya, je huoni kuwa haitakuwa hasara bali itakuwa ni faida? Kwani mapendo inaenda kwa umbali gani, hata tukiwa na maoni mengi mabaya, ya kupendelewa mbele ya ukweli wenyewe bila mapendo itawezekana? Tunaweza kufa bila ya maarifa ya ukweli mwingi na ilhali, kubebwa mapaja ya Abrahamu. Lakini kama tutakufa bila ya mapendo, nayo maarifa itatokana na nini baina yetu? Kama tu jinsi inavyo mukaribisha shetani na malaika wake!

> Mungu wa mapendo anatukataza tusiwahi kufuata nyayo zabo! Hebu na akaweza kutu tayarisha maarifa ya ukweli wowote, kwa kuyaza myoyo yetu na mapendo yake yote na furaha na amani yote mu kuamini.[53]

Ombi sawa sawa na hili linatuhitaji sisi kufanya nini, ao linatupatia sisi nini, wakati tunakuja mu kushughulikia kwetu ku mzozo?

Wesley anaongea hapa juu ya hali fulani yenye tunakuwa wanyonge na kuwa na roho wa woga, na hivyo basi wa ukatili na kutoeleweka; roho wa kuangamiza mawasilianao ya karibu sana yenye ni mapendo ya Mungu kwetu sisi. Mu kushikilia roho kama hiyo, tunaegemea kutafuta uhakika na usalama kwa kujigawa sisi wenyewe kutoka vyanzo vile banajulikana juu ya kutokuwa kwetu na uhakika. Pahari pa kusonga kuelekea kwabo mu tumaini ya kuelewa na kuweza pia nasi abo kutuelewa, tunasonga mbali, na kujenga picha juu yabo yenye itafafanua kukatala kwetu kwabo. Na tunajaribu kubashawishi bengine juu ya kutufuata sisi. Tunaweza kutumia mazoea ya kuleta uadui mu jaribio hili: kama tunaweza kushawishi bengine kuwa (bako batu bawili tu) "pande," zenye zinapingana moya kwa nyingine na zenye haziwezi kuriziana, na kama tutaweza kufanikiwa kwa kuonyesha pande hizi mbili mu njia kama hiyo kuwa moya wao tu njo mwenye kuwakilisha ukweli, haki, na maadili basi tuko mu njia ya kusababisha utengano wenye (tunatumai kabisa) utatupa amani.

Mu kukumbana na jaribio hili la kuishia kuwa na woga na ukatili, jambo moya lenye tunaweza kufanya ili kupinga haya yote si kujipata mu uadui huu yenye ili zoeleka lakini kuutambua (haijalishi kama ni mazungumzo yetu ya makini ao mu yale ya batu bengine), ili kuyakatala, na kukabiliana nayo vilivyo. Lakini kupatiya nguvu chochote kile chenye tunafanya kunafaa kuwa ujasiri wenye nguvu, kuwa nia ya Mungu ni kukusanya bitu byote pamoya mu Kristu (Baefeso 1:10), na ombi la zati la kutosimama mu njia ya kutimiza nia hiyo.

---

[53] John Wesley, "Utangulizi" wa *Mahubiri juu ya matukio mbali mbali*, kanda 1 (1746), mu *Mahubiri ya I*, haririwa na Albert C. Outler, *Kazi za John Wesley*, kanda 1 (Nashville: Abingdon Press, 1984), k. 107. Kigriki cha "kama funda la moshi" kimeweza kutafusiriwa na kushughulikiwa hapa.

## Maono ya Mambo ya Kanisa na Kanuni

Tukiongea kitheolojia, kanuni ya kanisa ni hali ya "mwenendo," mu utatu in the triad "Neno, Sakramenti, and Mwenendo" bitu byenye tulizungumzia zamani. Lazima iwe kuhusu njia ya mienendo ya kanisa mu maisha binafsi ya kuwajibika ili kutimiza mwito wake. Mwenendo, kama ulivyo mfano halisi na uliyo zidi mu kanuni zetu pamoya na mu mifumo mingine yake, haiwezi kutenganishwa na neno na sakramenti: inaongozwa (na neno hai) na kuendelezwa na kupatiwa nguvu siku zote na neema ya uwepo sakramenti wa Mungu.

Njiya yenye kanisa linaweka mienendo yake binafsi ya maisha kivyake ni hali ya ushuhuda wake mu duniya. Wakati kanuni yake inawezesha na kuonyesha uwazi ku nguvuza kuunda-jamii mu Roho Mtakatifu, wakati inahudumu jukumu la kanisa "kuendeleza umoya wa roho mu nguvu za amani" (Waefeso 4:3) kwa nguvu na uwazi kama huo wa kuletea mwanadamu uelewa mpya wa uwezekano wa maisha mazuri ya pamoya, basi itakuwa imetimiza kusudio lake.

Mu haya, kama vile iko mu mambo mengine, yawezekana kuwa salama kusema kuwa sisi mu Kanisa Methodiste Umoja bado hatujawasili mu shabaha hiyo (rejelea. Wafilipi 3:12). Kuna, hata hivyo mali mu ya mila yetu binafsi yenye inaweza kutuleta karibu sana na shabaha hiyo kama tungeyatumia kwa hekima sana.

Mu masomo yenye ilichapishwa mnamo 1998, bana sayansi wawili wa kisiasa walitambua kuwa, juu ya muundo mpana wa kijamii-kiuchumi na kitamaduni, Umethodiste Umoja mu Inchi ya Amerika mara nyingi unaegemea kuonyesha mseto wa maadili na matukio juuya maswala ya mazingira ya jamii yake, pahari pa kutoa ushuhuda wazi na wenye umoya ku jamii hiyo. [54] Lakini baligundua kuwa mufano sawa na huo wa uwakilishi wa maoni tofauti juu ya maswala yenye wasi wasi wa pamoya ata unapatia

---

[54] John C. Green na James L. Guth, "Methodiste Umoja na Utamaduni wa Amerika: Picha ya Kihesabu," *Methodiste yenye iliitwa na Batu: Fomu na Marekebisho ya Maisha Yabo*, imehaririwa na William B. Lawrence, Dennis M. Campbell, na Russell E. Richey (Nashville, Tennessee: Abingdon Press, 1998), kk. 27-52. Angalia haswa utangulizi na hitimisho ya insha, kk. 27-28 na 49-50, yenye manukuu haya yametolewa.

Umethodiste Umoja “uwezekano wa kuwa na misimamo mipana ya kijamii na vile vile nafasi zenye zilifumwa kwa pamoya mu ya mazingira ya kijamii,” na bakasonga mbele kupendekeza kuwa shughuli ya uzito huu yenye inawezekana kujumuisha muchango “maalum wa kanisa” mpaka maisha ya uma. Balisonga mbele na kupendekeza kuwa utambuzi wa ampaka hii ungehitaji kanisa kuboresha “taratibu zake za utengenezaji-sera,” ili “kuhimiza maendeleo ya makubaliano halisi pahari pa kuonyesha maoni ya hoja yenye inapingana. . . . Bamethodiste lazima batambue kuwa mariziano hayaibuki kutoka ku mseto kwa mazingaombwe, na kuwa inahitaji kujitolea kukubwa kwa kitalasisi na kwa kibinafsi ili kuyatimiza.”

Uangalizi na mapendekezo haya ya banasayansi wa kisiasa inaonyesha, mu lugha yenye si ya kithiolojia, bamoya bamoya sifa muhimu za hali tuna na kazi yenye ipo mbele yetu kama kanisa mu himaya ya kanuni. Ukuzi mkuu na utofautishi wa Kanisa Methodiste Umoja kote kote mu duniya tangu machapisho ya masomo yao unafanya tu hali na kazi hizi kuwa zenye zarura na ushawishi sana.

Sehemu yenye inatangulia, juu ya “mseto na mzozo,” ilitoa sampuli ya bamoya bamoya mali za Wesley zenye zinapatikana kwetu zenye zinahusu aina ile ya ukomavu wa kiakademia, kihisia, na kiroho wenye tunahitaji kama tutaweza kuwa mu hali nzuri na bora ya kuelekea ku maswala yenye tunakabiliana nayo na kuelekeza kwa sisi benyewe kwa kadri namna tunakabiliana nayo. Mengi sana yangeweza kusemwa na inahitaji kusemwa, mu muunganisho huo, lakini ufaavu wa mali haya juu ya maulizo ya kanuni ni wazi. Tunahitaji fomu za kanuni zenye zinaendana na kujitolea kwetu ku kuu: yani, fomu zinazo heshimu ule upana mkuu yenye inajumuisha neema ya Mungu yenye inaokowa, fomu zenye zinatambua na kuimarisha tabia badishi ya neema hiyo na fomu zenye zinahudumu pahari pa kugeuza, ukuzi wa jamii yenye haina hatia. Kuhusiana na hayo, hali mahususi zinazohusiana na kanuni ya Wesley zinahitaji kutiliwa maanani sana: hali ya mukutano wa Bakristu.

“Mukutano,” mu matumizi haya, unarejelea kwanza kabisa, si ku mukutano wala ku bale banao husika mu mukutano kama huo—mitazamo miwili yenye inaweza kujitokeza kwetu bila shaka ni matumizi leo ya

Methodiste Umoja, pahari pa mwenendo wenye Bakristu banafaa kujihusisha mu. Mu mufano mmoya,[55] John Wesley alirejelea mukutao wa Bakristo kama “mbinu za kitalasisi za neema,” yani, mwenendo yenye inaanzia ku Bakristu na yenye inafaa kuimarisha ukuzi wetu mu “utakatifu wa moyo na maisha.” Ni njia moya wapo yenye Mungu anatusaidia kujisaidia wenyewe kuelekea kwa ukomavu wa imani, tumaini na mapendo. Unahusisha mambo ya maombi, uchunguzi-nafsi yenye inafaa, juu ya “kuongea ukweli kwa mapendo” baina ya sisi benyewe, uwajibikaji na usaidizi wa pamoya, na utiliaji maanani kwa makini juu ya namna tunaweza kujiendeleza sisi wenyewe ku siku za mbele. Mwenendo wa mukutano wa Bakristu unaendelea kupitiya fomu nyingi bila kusahau mazungumzo ya moya ku moya, kati ya Bakristu, mikutano ya kikundi kidogo cha aina mbali mbali na makusudio mbali mbali na hata matukio makubwa sana kama vile yale ya makusanyika rasmi yenye ilipangiwa kuwa makutano mu “mazingira” ya Methodiste Umoja. Kwa hakika, mwenendo wa mukutano wa Bakristu ni kwa kiasi fulani hali ya karibu kila jambo lenye lina fanyika mu kanisa, hata kama ni la umu sana na la kumakinikia na kuendeshwa kwa njia muzuri sana mu ya ule upana finyu uliyo fikiriwa-vizuri kando ya hali na maeneo husika. Kama vile kumbukumbu namna zinaonyesha, makutano madogo kwa kiasi ya Wesley na ya bahubiri bake balihisusha mambo zabiti ya mienendo, hata kama mazingira yake ya kawaida kwa muundo mu ya kikundi cha mapema cha Methodiste, yalikuwa mikutano ya “madarasa” na “bendi” mu ya mazingira ya mu ya Methodiste. Mengi sana kama hayo inaweza kusemwa juu ya hali ilivyokuwa mu Umethodiste wa Amerika Kaskazini.

Namuna tunavyoweza kujitolea kwa njia muzuri sana juu ya mbinu hizi za neema mu kanisa la karne ya ishirini na moya, na haswa mu kufikiria kwetu juu ya kanuni, ni swali wazi, na lile lenye linastahili kutiliwa maanani kwa umakinifu.

---

[55]Angalia “Kumbukumbu za Mkutano Mkubwa” za 1763, mu *Vyama vya Methodiste: Kumbukumbu za mkutano*, ziliharirriwa by Henry D. Rack, *Kazi za John Wesley*, kanda la 10 (Nashville: Abingdon Press, 2011), kk. 855-858. Wimbo wa sifa wa 1782 na John Fawcett, “Ibarikiwa Kamba Inafunga” (UMH 557) yenye inanyesha bamoya bamoya ya kile “mukutano” unahusu, kwa mufano, “Tunachangiza matatizo ya kila mmoya wetu,mazigo yetu ya pamoya tunavumilia. . . .”

Kanisa ni zawadi ya Utatu wa Mungu. Hata ni jamii yenye ubinadamu sana na talasisi. Hali zote juu ya uhalisia wake zinahitaji kushugulikiwa kwa uzabiti mu akili ku mambo yetu yote tunafikiria na hatua. Tunatowa shukrani kuu Kanisa la Ulimwengu, na ku kanisa Methodiste Umoja kama sehemu fulani ya mwili yenye mwito wake binafsi wa kutimiza kama ishara na mtumishi wa mapendo yenye ina okowa ya Mungu ku mwanadamu kushuhudia ku na kuimarisha maisha ya ajabu, mapendo na sifa yenye ni mwito bora kwa kila mwanadamu. Lakini pia tunafanya vyema ata kukumbuka kuwa, "tuna una akiba hii mu vyombo vya duniya."

> Kwani Mungu, mwenye aliruhusu mwangaza kuangaza mu giza, ameangaza mu myoyo yetu, ili kuweka mwangaza wa maarifa mu utukufu wa Mungu mbele ya Yesu Kristu. Lakini tuna akiba hii mu vyombo za duniya, kuwa utukufu wa nguvu unaweza kuwa wa Mungu, na hata si wetu.[56]

---

[56] 2 Wakor. 4:6-7.

# Maulizo ya Maitikio ya Maajabu, Mapendo na Sifa

Komiti ya Maneno ya Mwenendo na Imani ya Kanisa (CFO) ya Kanisa Methodiste Umoja inalomba maoni yako wakati tunaendelea kuimarisha karatasi yenye itafasiri uelewa wa Methodiste Umoja wa asili ya kanisa. Nyuma ya kipindi cha masomo, kufikiria na mazungumzo ya CFO itaweza kusanifisha bruyon yake ya sasa na kuiwasilisha ku mkutano mkuu wa 2020 ili aweze kuchukua nafasi kando kando ya taarifa nyingine rasmi za kitheolojia juu ya kanisa. Maoni yako ni muhimu kwa ufanisi wa hatua hii.

Kama unaweza tungependelea utupe maoni yako kwa kutumia uchunguzi wa mtandaoni yenye inapatikana ku www.umc.org/CFOWonderLovePraise. (Uchunguzi wa mtandaoni umo mu lugha ya kiingereza. Tunahimiza bamemba ba makutano ya inchi la Amerika kuunda njia za ukusanyaji na upangilia wa maoni yenye itawafaa sana kwa kila mawazo wa mtu binafsi.) Kama huwezi kuyaza uchunguzi mtandaoni unaweza kuitikia maulizo yenye iko hapa chini na kutuma barua pepe ya maoni yako ku cfo@umc-cob.org.

Batu benye bamejihusisha mu makala ya masomo banaweza kuwasilisha uchunguzi ao maulizo ya maitikio abo binafsi ao unaweza kuwakusanyia matokeo ya kikundi yako na silishe moya wapo ya uchunguzi ao maulizo ya majibu kwa faili kwa kikundi yote. Tafazali elekeza maulizo yoyote yenye unaweza kuwa nayocfo@umc-cob.org.

## <u>Taarifa ya Jumla:</u>

**Jina:** **Umemba wa Mukutano:**

**Ninaijaza fomu hii ku jina la (ripoit moya):** mimi mwenyewe ku kikundi cha masomo kikubwa sana

**Kama unaripoti kwa niaba ya, ni batu batu bangapi kwa wastani benye balihuzuria vikao vyako vya masomo?**

**Ni nini *<u>kinafafanua</u>* muzuri sana wewe ao muundo wa kikundi lako kwa uhusiano na UMC?** *(Ripoti moya kutoka kwa kila kategoria; kama una ripoti juu ya kikundi fanya uchaguzi kutokana na wingi wa benye bali kuwemo kwa kikundi.)***:**

**Kategoria 1:** Balei Viongozi ba dini

**Kategoria 2:** Mwito uso-Kanisa Ameajiriwa na Baumini ba mu UMC

Ameajiriwa na Uajaenti Mkuu ao Tarasisi nyingine ya UM (iso-masomo)

Mwanafunzi wa Masomo ya kipastere Masomo ya Uchungaji ao Ualimu mwengine mu Kitabu cha Mwenendo cha Kitheolojia

***(Kama wewe si mutu wa Methodiste Umoja, wewe ni mumoya wa basaidizi betu ba umoja wa madini, ao memba ba zehebu lingine la Methodiste ao la Wesley, tafazali tuma barua ya mutandao cfo@umc-cob.org kwa maagizo ya majibu.)***

## Maulizo ya Maitikio:

**Mu kipimo cha 1-5, huku 1 ikiwa "ninakatala kabisa" na 5 ikiwa "ninakubali kabisa", tafazali jibu taarifa zifuatazo:**

Ninatambua Kanisa Methodiste Umoja mu makala yenye yamewasilishwa ku karatasi hii.

1 2 3 4 5

Kuna mazingira na mada muhimu ku UMC yenye karatasi hii haikuangaziya.

1 2 3 4 5

Karatasi hii inaweza kufunzwa mu jamii/mawazo yangu.

1 2 3 4 5

Mazingira, hali na maneno ya jumla ya karatasi yako wazi na rahisi kusikiya.

1 2 3 4 5

**Tafazali fafanua ku majibu yako juu ya maulizo yenye ili hapo yulu kwa kufurnir majibu mafupi ya zifuatazo:**

Mu njia gani njo weye unatambua UMC mu karatasi hii? Ni mazingira ao mada gani yenye inapatikana mu ayo yenye inaelezea kwa njia muzuri sana juu ya sisi ni nani kama batu na Methodiste Umoja?

Kuna kitu chochote yenye ni muhimu ku maisha ya UMC yenye inakosekana mu karatasi hii?

Ni mavigezomaalumu gani na/ama mitazamo gani mipya ya hati hii ambayo iliwapa motisha?

Ni kwa njia gani njo waraka unaweza kuendelesha ili kuongea kwa njia muzuri sana ku jamii yako/mawazo wako?

Ni hali ao mada gani inahitaji kufafanuliwa?

Basi, kuna maoni yoyote mengine yenye ungependa kutoa?